**Fursa**

**Brigedia Aloyce Mwanjile aasa vijana kuchangamkia korosho** Uk. 9

**Biashara**

**Dhahabu, utalii, usafirishaji vyatunisha fuko la dola** Uk. 18

**Jamii**

**Onyo la wasomi kuhusu maandamano** Uk. 22


# Pambazuko

Toleo Namba 174 Jumatatu, Julai 20-26, 2026


## Kamanda Tibaigana awatonya wastaafu Uk. 16



# Tanzania kutengwa ikipuuza

- Wasomi waonya kuhusu tishio linalotokana na matakwa ya Jumuiya ya Madola

Uk. 6&7

*Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, Abdel Fattah El-Sisi akiwapungia wananchi waliofika viwanja vya Ikulu, Dar es Salaam baada ya kuhitimisha ziara yake ya kitaifa juzi - Jumamosi., Julai 18, 2026. Alisindikizwa na mwenyeji wake, Rais Samia Suluhu Hassan. (Picha na Ikulu).*

# MO Sugar, Kagera wajivua sukari yenye mchanga



Uk. 12

## BoT: Deni la Taifa laelekea kwenye utulivu

Habari Uk.20

**Tafakuri ya Bagonza**

## Uanaharakati: CCM isikane urithi wake

Safu Uk. 10

Tahariri

# Viongozi wa dini, msivunje daraja la amani

JAMII imezoea kuona viongozi wa dini kuwa ni taa inayowaka wakati wa giza, sauti ya busara wakati wa hasira na daraja linalowaunganisha watu waliofarakana kwa sababu mbalimbali.

Ndiyo maana minyukano inapoibuka miongoni mwa viongozi hao, waumini na wananchi kwa ujumla hubaki na maswali mazito; "ikiwa wanaohubiri upendo, msamaha na maridhiano wanashindwa kuvumiliana, jamii itakimbilia wapi kutafuta suluhu?

Katika siku za karibuni, tumeshuhudia kauli zinazokinzana, lawama, mashambulizi ya maneno na hata makundi yanayovutana ndani ya taasisi za dini.

Tofauti za mawazo siyo dhambi; ni sehemu ya maisha na zinaweza kusaidia kujenga taasisi imara. Tatizo huanza pale tofauti hizo zinapogeuzwa silaha za kudhalilishana, kuchafuana na kugawa waumini.

Pambazuko tunaamini kuwa madhabahu, mimbari na majukwaa ya kiroho hayapaswi kuwa viwanja vya kulipizana kisasi wala majukwaa ya kuonyesha ubabe.

Viongozi wa dini wanapaswa kukumbuka kwamba nafasi walizopewa siyo mapambo ya heshima, bali ni dhamana nzito. Waumini wanawasikiliza, vijana wanawaiga na jamii inawategemea kusaidia kutuliza migogoro ya kifamilia, kisiasa na kijamii.

Wanapovurugana hadharani, siyo wao pekee wanaopoteza heshima, bali wanadhoofisha imani ya wananchi katika taasisi walizokabidhiwa kuziongoza.

Mbaya zaidi, migawanyiko ya kidini inaweza kutumiwa na watu wenye maslahi binafsi kueneza chuki, ukabila, udini au misimamo ya kisiasa inayohatarisha amani.

Historia imetufundisha kwamba maneno yanapotolewa bila kiasi, yanaweza kuwasha moto ambao kuuzima hugharimu maisha, mali na mshikamano wa taifa. Hivyo, kila kiongozi wa dini anapaswa kupima kauli zake na kujiuliza kama zinajenga, zinaponya na kuunganisha, au zinabomoa.

Sisi tunawahimiza viongozi hawa kurudi kwenye misingi ya imani wanazozihubiri; unyenyekevu, upendo, ukweli, uvumilivu na msamaha. Migogoro yao ishughulikiwe kupitia vikao vya ndani, mazungumzo ya dhati na taratibu zinazokubalika, siyo kupitia mitandao ya kijamii, mahubiri ya vijembe au mikutano ya kushambuliana.

Kukaa pamoja hakumaanishi kukubaliana katika kila jambo; kunamaanisha kutambua kwamba tofauti zinaweza kusimamiwa bila kuvunja utu na heshima.

Ni muhimu pia waumini kutokubali kutumiwa kama askari wa makundi yanayohasimiana. Imani haipaswi kuwafanya watu wafumbe macho mbele ya kiburi, ubaguzi au matumizi mabaya ya madaraka.

Waumini wana haki ya kuhoji kwa heshima na kuwataka viongozi wao kurejea kwenye wajibu wao wa kiroho na kijamii ili kuendelea kulinda heshima zao na taasisi wanazoongoza.

Wakati huohuo, serikali – kupitia vyombo vyake, inapaswa kuhakikisha sheria inalinda usalama, usawa na haki ya kila mmoja, wakiwamo viongozi wetu wa dini ili kudhibiti jinai.

Aidha, mabaraza ya dini na taasisi husika yanapaswa kuweka mifumo madhubuti ya usuluhishi na maadili.

Viongozi wanaokiuka mipaka wawajibishwe kwa haki, bila upendeleo, ili kulinda hadhi ya taasisi na matumaini ya waumini.

Taifa linahitaji viongozi wa dini wanaokuwa chemchemi ya faraja, siyo chanzo cha hofu; wajenzi wa madaraja, na kamwe siyo wale wanaobomoa.

Wakati umefika sasa viongozi wa dini waache kuvurugana, warejeshe uaminifu na waongoze kwa mfano. Amani wanayoihubiri lazima ionekane kwanza katika maneno, matendo na uhusiano wao wenyewe.

# Kambi maalum ya matibabu...



*Mbunge wa Arusha Mjini na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Paul Makonda, akifuatilia shughuli za matibabu ya kibingwa kwenye kambi maalum aliyoiasisi jijini Arusha. Kambi hiyo ya siku saba, hadi jana ikihitimishwa imetibu wagonjwa zaidi ya 20,000. (Picha na Mpigapicha Maalum).*

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**


## TIMU YA PAMBAZUKO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mhariri Mkuu** | : | Simon **MKINA** | (simon@pambazuko.or.tz) |
| **Mhariri Mtendaji** | : | Peter **NYANJE** | 0784 211 716 |
| **Mwandishi Mkuu** | : | Elizabeth **HOMBO** | 0712 792 216 |
| **Mwandishi Mwandamizi** | : | Andrew **MSECHU** | 0769 415 815 |
| **Mkuu wa DTP** | : | Yassin **LUPATU** | 0782 009 971 |
| **Mkuu wa Utawala** | : | Tryruckia **MFINANGA** | 0744 768 263 |

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*


# Dunia: Hapa na Pale

## Trump amkataa tena Epstein

MZIMU wa bilionea Jeffrey Epstein, aliyefariki dunia gerezani mwaka 2019 katika mazingira yaliyotajwa rasmi kama kujiua, umeendelea kumkaba Rais wa Marekani Donald Trump.

Epstein (pichani) alikuwa anakabiliwa na mashtaka mazito ya kusafirisha binadamu na kuwanyanyasa kingono wasichana wadogo.

Rais Trump amesema madai ya kuwa karibu na Epstein hayana msingi, akisisitiza kuwa alijitenga naye mapema na hakuhusika katika vitendo vyake.



Kauli hiyo imekuja huku kukiwa na shinikizo la umma kutaka uwazi zaidi kuhusu mitandao ya Epstein na uhusiano wake na watu wenye mamlaka. Hoja hiyo imeendelea kugawanya maoni, huku wachambuzi wakitaka ukweli kamili uanikwe hadharani kwa maslahi ya haki.

## Anayedaiwa jasusi anyongwa

RAIS mmoja wa Iran amenyongwa na serikali ya nchi hiyo kwa madai kwamba alikuwa akitumiwa na Israel kusaka taarifa za taifa hilo la Kiislam. Alinyongwa Jumatano iliyopita.

Mahakama ya Iran, ambayo inaelezwa kutekeleza matakwa ya serikali, ilitoa taarifa kwamba mwanaume huyo, Hamidreza Sabet Esmaeilipour amenyongwa baada ya kuthibitishwa kuwa alikuwa jasusi wa Israel.

Kutokana na uhasama wa miaka mingi na Israel, Iran imekuwa ikiwanyonga raia wake ambao inashuku wanafanya ujasusi kwa kutumwa na Israel dhidi ya nchi yao.

Taarifa zinaeleza kuwa Hamidreza alitiwa nguvuni na vyombo vya dola Aprili 29, 2025 na alinyongwa wiki iliyopita baada ya kupatikana na hatia ya kutekeleza ujasusi akitumwa na nchi hasimu dhidi ya Iran.



## Traore: Wote tukatae rushwa

KIONGOZI wa Burkina Faso, Ibrahim Traoré, amesema serikali yake imefanikiwa kukomesha vitendo vya rushwa vilivyokuwa vimekithiri katika taasisi za umma, akisisitiza kuwa hatua hiyo imeimarisha uaminifu wa wananchi kwa serikali.

Traoré amesema mageuzi ya kiutawala, ukaguzi mkali wa matumizi ya fedha za umma na hatua kali dhidi ya watumishi wasiowajibika, vimeleta mabadiliko makubwa.

Aliongeza kuwa uwazi katika miradi ya maendeleo umeongezeka na mapato ya serikali sasa yanatumika kwa manufaa ya wananchi.

Rais huyo alieleza kuwa mapambano dhidi ya rushwa yataendelea kuwa kipaumbele ili kujenga taifa lenye nidhamu, uwajibikaji na maendeleo endelevu kwa watu wote.

## Afya ya Dkt Besigye teketeke

BADO afya ya kiongozi wa chama cha upinzani nchini Uganda, Dkt. Kizza Besigye ni mbaya.

Taarifa iliyotolewa kwa umma na chama chake cha PFF inaeleza kuwa katikati ya wiki hii, hali ilibadilika na kulazimu maofisa wa magereza, wakiambatana na wenzao kutoka idara ya usalama kumpelekea hospitali, huku wakijitahidi kuficha kuvuja kwa taarifa hizo.

Besigye, kiongozi ambaye amekuwa gerezani kwa muda sasa, Jumanne iliyopita alitolewa gerezani kwa siri, na kupelekwa kwenye hospitali ambayo bado serikali inaficha kuitaja, lakini baadhi ya maofisa usalama wamevujisha taarifa za kuugua kwake, bila kutaja alikopelekwa kwa matibabu.

Hata hivyo, inaaminika kuwa amelazwa kwenye hospitali moja ya serikali inayotumika kutibu viongozi.

Na Mzee TAI

# Tukimbize laana ya rasilimali zetu

INAFURAHISHA sana kuishi kwenye nchi ambayo ukienda kulala, unalalia kitanda chenye godoro lililonakshiwa kwa tanzanite na shuka lenye upindo uliofumwa kwa vipande vidogo vya dhahabu.

Hata hivyo, pamoja na kupata usingizi juu ya utajiri huo, ukiamka asubuhi unakunywa uji wa muhogo usio na sukari kwa sababu huna mia mbili ya kiberiti.

Nchi yangu ina miujiza ya kipekee duniani; nchi pekee ambapo madini ya nadra hayapatikani popote kuanzia Tokyo hadi New York, lakini wananchi wake walioko mita chache kutoka machimbo hayo bado wanaomba msaada wa vyandarua vyenye dawa kutoka kwa wafadhili.

Hivi kweli tumerogwa, au huyu mganga aliyeturoga alikufa na ufunguo wa akili zetu?

Wakati mwingine akili yangu inasema kudhani kwamba tumerogwa ni kuwasingizia bure wachawi, lakini ukweli mchungu uliopo, na unaouma zaidi, ni kwamba hatujarogwa na mtu yeyote kutoka nje; tumeamua kujiroga wenyewe kwa kuwafuga "mchwa" wa kisasa wenye suti na tai.

Mchwa hawa hawali mbao tena; wamehamia kwenye karatasi za mikataba na akaunti za benki. Wana uwezo wa ajabu wa kuhomola kila senti inayotokana na jasho la madini yetu na kuihamishia kwenye akaunti za siri kule Dubai, Uswisi na Visiwa vya Jersey, ambako wanaficha fedha walizochuma kutoka hapahapa.

Kutokana na mchwa hawa kuenea kila mahali, nimepata wasiwasi endapo yale yaliyomo kwenye Dira ya Maendeleo ya 2050 yatafikiwa.

Nimesoma na kutafakari yaliyomo kwenye dira hiyo. Hakika ni waraka mzuri sana, ulioandikwa kwa lugha yenye maneno ya kuvutia yaliyosheheni namba na chati za kupendeza, lakini napata shida kidogo na kujiuiza; "katika mazingira haya ambapo mchwa wanaendelea kutafuna, dira hii itafikiwa kweli?"

Au nayo itafuata nyayo za dira zilizopita na kwenda kupumzika kwa amani kwenye makabati, ikisubiri kufutwa vumbi na vizazi vi-



javyo vinavyokuja kushangaa jinsi babu zao walivyokuwa mabingwa wa kupanga lakini wazito wa kutenda?

Kama tunataka dira hii isigeuke kuwa hadithi ya Alfu Lela Ulela, ni lazima tuchukue hatua za makusudi na za busara kuliko maneno tupu na yafuatayo yafanyike.

Lazima tutengeneze viuatilifu vikali vya kisheria na kiuwajibikaji ili kuwateketeza mchwa hawa waliojificha ndani ya mifumo yetu. Hakuna maendeleo yatakayofika ikiwa kila shilingi ya madini na kodi inaishia mifukoni mwa watu wachache wanaoshindana kwa ukwasi.

Kwamba wakati umefika sasa kuacha mikataba ya kificho inayofanywa gizani. Kila tone la madini linalotoka ardhi yetu lazima lilete shule bora, hospitali zenye dawa, na barabara za kisasa, na siyo sifa zisizoweza kuimarisha maendeleo ya kila kaya.

Ni muhimu sasa kuhimiza ujenzi wa viwanda vya ndani ili kuchakata madini yetu badala ya kusafirisha udongo na madini ghafi nje ya nchi. Ni lazima sasa tuchongee na kusafisha madini yetu hapa nyumbani ili kutengeneza ajira za kweli kwa vijana wetu.

Ni muda wa kuamka sasa kutoka kwenye usingizi huu wa pono. Hatuwezi kuendelea kuwa walinzi wa utajiri wa dunia huku wenyewe tukitembea vifua wazi na kukabwa kwa njaa.

Historia mpya lazima iandikwe sasa na kukemea laana ambayo inaweza kutufika kwa baadhi yetu kuendelea kuhomola rasilimali zetu kwa manufaa binafsi.

Habari Kuu

# Tanzania kutengwa ikipuuza




*Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu akiwa mahakamani*

Na Mwandishi WETU

TANZANIA inaweza kutengwa na Jumuiya ya Madola iwapo itapuuza maagizo yaliyotolewa na kamati ya mawaziri ya jumuiya hiyo hivi karibuni.

Mbali na jumuiya hiyo, washirika wake na taasisi zinazohusiana nayo, huenda zikafuata hatua zitakazochukuliwa.

Hayo yameelezwa na mwanasheria nguli nchini, Dkt. Rugemeleza Nshalla wakati akizungumzia athari mbalimbali zinazoweza kuipata Tanzania endapo itadharau au kushindwa kutekeleza masharti iliyopewa na Jumuiya ya Madola kupitia tamko lake la Julai 10, 2026.

Dkt. Nshalla amesema hayo mwishoni mwa wiki wakati akijadili maagizo ya Jumuiya ya Madola waliyoyatoa kwa Tanzania Julai 10, 2026.

Tamko la Mawaziri wa Jumuiya ya Madola (CMAG) limetolewa baada ya kupokea taarifa rasmi kutoka kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo na Mjumbe maalum, Rais wa zamani wa Malawi, Dkt. Razarus Chakwera aliyefanya ziara nchini Tanzania ambapo alikutana na viongozi wa vyama vya siasa, asasi za kiraia na wadau wengine kadhaa kuhusu yaliyojiri wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025.

Katika tamko hilo CMAG imeipa Tanzania ratiba ya siku 30, 60 hadi 90 kutekeleza maagizo kadhaa, ambapo kati ya hayo, ni kuachiwa huru kwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrsia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu ndani ya siku 30.

Lissu yupo gerezani akikabiliwa na mashtaka ya uhaini ambayo hayana dhamana. Anadaiwa kula njama za kuipindua serikali.

Aidha, CMAG imepanga kufanya kikao maalum Septemba mwaka huu kupokea taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa mapendekezo yake na kueleza wazi kuwa itazingatia hatua zaidi iwapo maendeleo yanayotarajiwa hayatapatikana.

Katika ufafanuzi wake, Dkt. Nshalla, ambaye pia ni Mwanasheria Mkuu wa Chadema, anasema endapo Tanzania haitatimiza masharti hayo, ipo hatarini kupoteza hadhi ya taifa linaongozwa kiungwana, kistaarabu na litawekwa kwenye orodha ya mataifa yanayoongozwa na wababe, na watu wasioheshimu tamaduni za kidemokrasia.

Anasema nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola zinaweza kuanza kuiwekea vikwazo Tanzania, kama ilivyowekewa Zimbabwe chini ya Rais Robert Mugabe.

Inaendelea Uk. 7

# Tanzania kutengwa

Inatoka Uk. 6

Ingawa serikali ya Tanzania haijazungumzia tamko hilo hadharani, pamoja na mambo mengine, CMAG imeipongeza serikali kwa kuruhusu mjumbe maalum wa jumuiya hiyo kufanya kazi zake kwa uhuru na kukiri kuwa baadhi ya masharti yaliyowekwa mwaka 2025 yameanza kutekelezwa.

Katika hoja zingine, CMAG imezungumzia uhuru wa mikutano, vyombo vya habari, mazungumzo ya vyama vya siasa, mifumo ya uchaguzi na uwajibikaji kuhusu matukio ya vurugu za Oktoba 29,2025.

Misingi mingine iliyozungumzwa na jumuiya hiyo ni pamoja na utawala wa sheria, haki za binadamu, uhuru wa kujieleza na uchaguzi wenye ushindani.

Mhadhiri wa Siasa za Kimataifa na Utawala wa Umma kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dkt. Richard Mbunda, amesema endapo Tanzania haitafuata maagizo ya jumuiya hiyo itakuwa ni kibano cha kidiplomasia.

Amesema Tanzania ilipata heshima kwa miaka mingi, sasa inapoanza kunyooshewa kidole na jumuiya hiyo yenye nchi 56 inafanya hali yake kidiplomasia iwe mbaya zaidi.

"Huko nyuma kuna nchi kama Pakistan na Zimbabwe zilisimamishwa na Jumuiya ya Madola kutokana na mambo kama haya ya kidemokrasia, sasa sisi hatutaki tufikishwe huko tunaamini serikali itatekeleza maagizo hayo," amesema Dkt. Mbunda.

Mwanazuoni huyo amesema ingawa hategemei Tanzania kuondolewa kwenye jumuiya hiyo, lakini kusimamishwa tu italeta madhara makubwa.

"Endapo Tanzania itasimamishwa tutashindwa kunufaika na huduma zinazotokana na Jumuiya ya Madola ikiwemo ufadhili na hisani nyingine ikiwamo za elimu na mengineyo..."

"Lakini pia Tanzania itaonekana kama taifa lililoshindikana kufuata matakwa ya demokrasia ikizingatiwa pia kuna msukumo kutoka mataifa


Dkt. Richard Mbunda

mengine makubwa,"alisema Dkt. Mbunda.

Julai 16, 2026, Asasi za kiraia nazo zilitoa tamko lao wakihimiza serikali kufanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na Jumuiya ya Madola.

Akisoma tamko hilo kwa niaba ya asasi hizo, mchumi na mchambuzi wa masuala ya siasa, Bubelwa Kaiza alisema Tanzania inahitaji ukweli, haki na uwajibikaji.

"Hali ya usalama, amani, haki na uwajibikaji nchini Tanzania imekuwa tete tangu siku ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 29, 2025, tunaitaka mamlaka ifanyie kazi mapendekezo yaliyotolewa na Jumuiya ya Madola,"amesema Kaiza.

Pamoja na hayo, Julai 13,2026 akizungumza kwenye mkutano wa mawakili, Rais Samia Suluhu Hassan, alisema Tanzania ni bora kwenye kufuata haki za binadamu.

Akifafanua baadhi ya malalamiko yaliyopo kuhusu uvunjifu wa haki za binadamu, mkuu huyo wa nchi alisema ni hujuma kutokana na kasi ya ukuaji wa Tanzania.

Inaendelea Uk. 8

## Habari Kuu

# Tanzania kutengwa

Inatoka Uk. 7

"Kwa upande wetu sisi Tanzania, kwa muda mrefu tunaangalia haki za binadamu. Sasa haya yanayosemwa na mengine yatakayoendelea kusemwa, sisi tunajua jinsi tulivyo bora, lakini hata ulimwengu unajua," ameeleza Rais Samia.

Katika kile kinachoonekana kama amejibu matamko ya hivi karibuni yaliyotolewa na mataifa makubwa ya nje, Rais Samia alieleza kuwa baadhi ya mataifa yanaangalia njia ya kurudisha nyuma mataifa yanayoendelea na hoja haki za binadamu, ni moja ya jambo linaloibuliwa kwa mantiki hiyo.

"Jinsi nchi zetu hizi zinazoendelea, tunavyokwenda mbele, wengine wanaangalia njia na mbinu za kutuvuta nyuma ili tusiende kwa kasi ile ambayo tunakusudia…"

"Tunashuhudia mataifa yakihujumiana. Tunashuhudia vijana kulaghaiwa na kumezeshwa sumu dhidi ya mataifa yao na kushawishiwa kuhujumu chumi zao zilizojengwa kwa nguvu kubwa…"

"Vilevile kuna wimbi la kuwaaminisha vijana kwamba serikali zao hasa za Afrika hazifuati au zinakiuka haki za binadamu," aliendelea kufafanua.

Akifafanua zaidi Rais Samia ameeleza kuwa haki za binadamu zimewekwa katika Katiba na Sheria za Tanzania na kwamba wananchi wakiwa na malalamiko wanaweza kwenda Mahakamani na kupata haki zao. "Hata ulimwengu unajua sisi tuko wazuri namna gani au kiasi gani katika kuangalia haki za binadamu. Ila wanasema mpe mbwa jina baya ili ufanyaje, umuue…"

"Sisi Tanzania tuko vizuri kwenye haki za binadamu na uzuri ni kwamba hakuna aliye juu ya sheria zetu zilizowekwa. Hizo haki za binadamu zilizowekwa kwa sheria na sheria nyingine zozote, hakuna aliye juu ya sheria zetu. Anayevunja sheria atashughulikiwa," alisisitiza.

### Historia ya Tanzania na Jumuiya ya Madola

Tanzania (wakati huo ikiitwa Tanganyika) ilijiunga rasmi na Jumuiya ya Madola mwaka mwaka 1961 baada ya Tanganyika kuwa huru.

Siku chache baada ya kujiunga, Tanganyika iliishinikiza Afrika Kusini kujiondoa kwenye jumuiya hiyo kutokana na vitendo vyake vya ubaguzi wa rangi wakati huo, na nchi hiyo iliondolewa.



*Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola, Rais wa zamani wa Malawi, Dkt. Lazarus Chakwera, akiwa katika picha ya pamoja viongozi wa Chadema.*

# Brigedia Mwanjile aasa vijana kuchangamkia korosho




**Na Mwandishi WETU**

MWENYEKITI wa Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Brigedia Jenerali (mstaafu), Aloyce Mwanjile amewaasa vijana kuchangamkia kilimo cha korosho, badala ya kulalamika ukosefu wa ajira.

Amesema kilimo cha korosho ni mkombozi wa uhakika kwa Tanzania, ikiwa vijana wengi ambao bado wana nguvu "watakichangamkia" mapema.

Mwanjile amesema kwamba mazingira ya sasa ya kilimo hicho yanavutia kwani serikali imeweka nguvu na utaratibu wa kuinua zao la korosho.

Amesema kupitia ushirikiano ambao serikali imekuwa ikiwapa wakulima wa korosho, ikiwamo pembejeo za ruzuku na elimu kwa wakulima, uzalishaji wa zao hili umeendelea kuimarika.

Brigedia huyo mstaafu ameyasema hayo wiki iliyopita wakati akizungumza na CMG akiwa shambani kwake Litunu, wilayani Ruangwa mkoani Lindi.

"Vijana wana fursa kubwa ya kuwa matajiri kupitia kilimo cha korosho, na sasa hivi zao hilo linaanza kuleta faida ndani ya muda mfupi, hivyo niwaombe Watanzania wasiache nafasi hii ya kuufukuza ufukara," alisema Mwanjile.

Mwenyekiti huyo ambaye ni mkulima na mbanguaji wa zao la korosho, amesema aliamua kuingia kwenye kilimo hicho baada ya kustaafu na kuamini kuwa atafanikiwa, hivyo kuwa mfano halisi wa manufaa ya kilimo.

Amesema kiongozi anayetoa maelekezo kwa wakulima anapaswa pia kufahamu kwa vitendo kila hatua ya uzalishaji, ili aweze kujibu maswali kwa usahihi na kutoa elimu yenye tija.

Akizungumzia faida za kuuza korosho zilizobanguliwa badala ya kuuza zikiwa ghafi, Mwanjile alisema mkulima anapata faida kubwa zaidi.

"Kwa mfano korosho ghafi tani moja ningeuza kwa Shilingi milioni 2.5, lakini hiyohiyo tani moja nikiibangua, nikaikausha nakwenda kupata Shilingi milioni 5..."

"Hivyo maana yake nimepata faida mara mbili lakini pia unapobangua unaanzisha ajira, vijana wanaonisaidia wote hapa kwao ni ajira na wao maana yake maisha yao yataboreka," amesema.

Amewataka wakulima kuendelea kuwa wasikivu na kufuata maelekezo ya maofisa ugani ambao wameajiriwa na Bodi ya Korosho Tanzania katika kata zote zinazolima korosho.

Akizungumza juu ya hali ya upatikanaji wa sulfur katika msimu huu, amewataka wakulima kuwa na imani na matumizi ya viuatilifu vya maji vilivyoidhinishwa, ambavyo pia vina uwezo mkubwa wa kudhibiti magonjwa na kuongeza uzalishaji.

Brigedia Mwanjile amesema haitoshi tu kuisifia sekta ya kilimo kuwa imeajiri zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania, lakini wanapaswa kuiona sekta kama fursa ya kuboresha maisha yao na kuinua uchumi wao na kuleta ustawi wa kijamii.

Amehimiza vijana kuwa sasa ni wakati wao wa kutambua fursa zilizopo katika sekta ya kilimo na kuzitumia kujiletea maendeleo ya kiuchumi.


Lakini akatoa ushauri kwa serikali kuendelea kuweka mazingira rafiki na kuwawezesha vijana kuingia katika kilimo cha kisasa.

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA

# Uanaharakati: CCM isikane urithi wake



Mwalimu Julius Nyerere

HERUFI "M" katika jina la CCM ni Mapinduzi, yaani kilele cha juu kabisa cha harakati. Ukiondoa "Mapinduzi" katika jina hilo, CCM kinabaki ni chama mamluki kilichojaa ukandamizaji na dhuluma. CCM ni chimbuko la harakati. Tujikumbushe:

Kwamba, baada ya kuachana na starehe katika chama cha TAA, ilizaliwa TANU iliyokuwa na lengo la kuondoa ukoloni na kuleta uhuru. Hizo ni harakati.

Kwamba, kule Zanzibar, ASP ilifanya mapinduzi matukufu Januari 1964 na kuleta uhuru wa kweli. Zilikuwa ni harakati.

Kwamba, mwaka 1967, TANU ilizindua Azimio la Arusha baada ya kukiri kuwa "tumenyonywa vya kutosha na sasa tunataka mapinduzi ili tusinyonywe tena." Azimio la Arusha lilipindua meza na kuwafanya watwana kuwa mabwana. Hizo ni harakati.

Kwamba, mwaka 1977, TANU na ASP viliungana na kuunda CCM. Chama chenye historia ya kumwaga damu (ASP) kikaungana na chama chenye historia ya kudai haki kwa fikra kali na pevu (TANU). "Mapinduzi" ilikuwa ni alama wazi iliyowakilishwa na jembe na nyundo katika utambulisho wake. Ni harakati bado.

Kwamba, muundo wa CCM na medani zake za utendaji vilikuwa ni vya kiharakati (Vangardism). Chama kilishika hatamu na kutoa miongozo iliyopikwa na makada waliojaa uyakinifu. Nadharia iliongoza matendo daima. Hizo ni harakati.

Kwamba, imani 10 za TANU na CCM zilisisitiza uzalendo kwa taifa isipokuwa moja tu iliyosisitiza utii kwa rais. Haki na Ukweli zilikuwa tunu kuu za chama. Amani haikuzungumziwa kwa sababu ni zao la tunu. Hizo ni harakati.

Kwamba, TANU na CCM ile ilikiri uwezekano wa kukosea nadharia au matendo na kujisajihisha. Iliamini kujisahihisha ni hatua muhimu ya kuimarika na siyo kudhoofika. Mwana harakati huamini katika uwezekano wa kuanza upya baada ya kugundua amekosea.

Kwamba, chini ya TANU na CCM ya kianaharakati, ulinzi na usalama wa taifa ulikuwa mikononi mwa wananchi. Vyombo vya ulinzi vilikuwa ni watumishi wa wananchi na si mamluki wa serikali dhidi ya wananchi. Kila mwananchi alikuwa ni "Usalama wa Taifa". Hicho ni kiwango cha juu cha harakati.

Kwamba, neno Haki na Utu yalikuwa ni msingi wa nadharia ya hotuba na maandiko ya TANU na CCM. Kila penye dalili ya dhuluma ulimkuta TANU na CCM upande wa wanyonge. CCM imelipwa kiasi gani kuacha kutumia maneno haya kwa fahari na kifua mbele? Bila neno Haki unafarakana na harakati.

Kimsingi, CCM ndiye baba wa harakati, nguzo ya Haki na mpinga dhuluma popote duniani. Isimame ihesabiwe na isiwaache wapinzani kujitwalia utukufu kwa tunu za CCM.

Yaliyotupata yote ni kwa sababu tumeacha na kubeza harakati. Taifa lisilo na harakati ni sawa na pango la wanyang'anyi. Wanyonge ni kitoweo cha wenye nguvu. Taifa linajengwa na wenye moyo na kuliwa na wenye meno.

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***



Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA


Kona ya Dkt. Bisimba

# Iweje sauti zifanane kuhusu Tanzania?

JULAI 10, 2026, Jumuiya ya Madola (Commonwealth Ministerial Action Group- CMAG), ilitoa tamko baada ya mkutano wake wa 73 ikiweka msisitizo kwa Tanzania kuchukua hatua kuimarisha demokrasia, utawala wa sheria na haki za binadamu.

CMAG pamoja na hoja nyingine iliitaka Tanzania kuachilia au kuhakikisha haki za kisheria za viongozi wa siasa wanaoshikiliwa, akiwemo Tundu Lissu, kwa mujibu wa sheria na viwango vya haki.

Hili siyo tamko la kwanza la aina hii kwani tumewasikia Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), Marekani pamoja na baadhi ya taasisi za kimataifa, zote zikionyesha wasiwasi kuhusu mwenendo wa haki za binadamu, uhuru wa kisiasa na mazingira ya chaguzi zilizopita.



Imebidi nijiulize kwa nini hawa washirika wa Tanzania wanatoa ujumbe unaofanana? Hivi inaweza kuwa ni bahati mbaya kuwa Jumuiya ya Madola, EU na Marekani wazungumze mambo ya kufanana?

Kwa kawaida, matamko ya aina hii huibua hisia tofauti. Wapo wanaoyaangalia kama ushauri wa kirafiki unaolenga kusaidia nchi kuimarisha mifumo yake ya utawala wa sheria.

Kuna wanaotafsiri kama ni kuingiliwa kwa mambo ya ndani ya nchi. Hapa panatosha kusimama na kuendelea kuhoji tena iweje sauti kutoka maeneo tofauti zibebe ujumbe huo huo?

Hakuna ubishi kuwa kila nchi ina mamlaka ya kujiamulia mambo yake ikiwa ni msingi wa uhuru wa taifa hilo.

Hata hivyo, tukiangalia upande mwingine tunaiona Tanzania iliyojiunga kwa hiari na Jumuiya ya Madola, Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na hata SADC kuwa sehemu ya taasisi hizi kunaambatana na ahadi za kuheshimu misingi iliyowekwa ikiwemo utawala wa sheria, haki za binadamu na utawala unaowajibika.

Hivyo, basi matamko yanayotolewa hayapaswi kutazamwa kuwa ni shinikizo kutoka nje kwani Tanzania ni sehemu ya taasisi hizo na nyingine ni wabia wake.

Matamko hayo ni ukumbusho wa ahadi ambazo nchi wanachama walizikubali. Tunachotakiwa kuangalia zaidi siyo iwapo mtoa tamko anatoka nje au ndani ya nchi bali yanayosemwa yana ukweli unaopaswa kutafakariwa.

Hata tukiangalia ndani tumeona watu mbalimbali wasomi, wanasiasa na hata raia tu wakizungumzia hayo ikiwemo kuachiwa kwa Tundu Lissu pamoja na kuwa wanaosema hivyo wanajua alikamatwa na yuko mahakamani hivyo sheria ingeachwa ifuate mkondo wake.

Shida ni kuwa huo mkondo wa sheria umenyooka? Inatakiwa busara ya hali ya juu kupima yasemwayo bila kumhukumu mtoa hoja.

Tanzania kwa muda mrefu ilijijengea heshima katika mchango wake katika amani, diplomasia na mshikamano wa Afrika.

Heshima hiyo ni mtaji mkubwa uliopaswa kulindwa. Kulinda mtaji si kwa kukataa kila ukosoaji unaoelekezwa kwetu, bali kujitahidi kuimarisha taasisi za haki, kuongeza uwazi katika utendaji wa umma na hali bora isiyo ya hofu kwa wananchi kutoa dukuduku zao.

Tunapaswa kama Taifa kujiuliza, je lipo jambo tunaloweza kufanya ili Tanzania yetu iendelee kujenga sifa yake njema badala ya kila wakati kupokea matamko ya shutuma?

Swali hili huenda likawa bora kuliko mabishano ya nani kasema nini. Tunapoona sauti kutoka pande mbalimbali duniani zinazohusu nchi yetu, tujiulize kwa tafakari ya kina kwa nini wote hawa waseme hivi na pia tuisikilize sauti ya watu wa nchi hii, kwani sauti ya watu ni sauti ya Mungu.

***Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.***

Habari

# MO Sugar, Kagera wajivua sukari yenye mchanga



Na Mwandishi WETU

UKWELI kuhusu nani aliyeingiza na kusambaza sukari inayolalamikiwa kuwa na mchanga, umeendelea kuwa siri, huku hofu kwa watumiaji wa bidhaa hiyo muhimu, ikiongezeka.

Usiri huo unaendelea kuimarisha hofu, hasa kutokana na dhana miongoni mwa watumiaji kuendelea kutilia shaka usalama wa afya zao, kwa maelezo kuwa iwapo sukari hiyo yenye viambata vya mchanga inaendelea kuwa sokoni, ni nani mwenye uhakika wa kutokuwepo viambata vingine vyenye madhara kwa binadamu?

Katika toleo lake la Julai 13-19 mwaka huu, gazeti hili liliandika habari ikieleza kuhusu hofu iliyotanda miongoni mwa wananchi kuhusu uwepo wa sukari yenye masalia ya mchanga ambayo imekuwepo sokoni kwa zaidi ya miezi miwili, huku Mamlaka ya Viwango nchini (TBS) ikithibitisha kubaini tatizo hilo na kuwa tayari ilishaagiza kampuni zilizoingiza sukari hiyo kusitisha usambazaji wake.

Kuhusu kampuni zinazohusiswa na uingizaji wa sukari hiyo, TBS ilieleza kuwa suala hilo ni siri kwa kuwa wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa taratibu zinazowaongoza.

Uchunguzi uliofanywa na Pambazuko ulibaini kuwa ipo kampuni moja inayotajwa kuingiza sukari hiyo kutoka nje ya nchi na kuifunga kwenye mifuko jijini Dar es Salaam.

**Kagera Sugar**

Katika ufuatiliaji uliofanywa na gazeti hili, Ofisa Masoko na Usambazaji wa Kampuni ya Sukari ya Kagera, Laurent Musai alieleza kuwa hana taarifa kuhusu uwepo wa sukari hiyo na kwamba hata hivyo, yeye siyo msemaji wa masuala yote ya kampuni na anachoweza kueleza yeye ni kuhusu sukari inayozalishwa ndani tu.

“Mimi kwa nafasi yangu, ninachoweza kuzungumzia ni kuhusu sukari tunayozalisha hapa tu. Katika hayo mengine mimi ni mtu mdogo sana, ukiweza mtafute Ofisa Mtendaji Mkuu (CEO) ndiye anayeweza kuzungumzia hilo, naomba tuishie hapo, kwaheri,” alisema ofisa huyo na kukata simu. Juhudi za kumpata CEO hazikuzaa matunda.

Hata hivyo, mmoja wa wakurugenzi wa kampuni hiyo ambaye hakupenda kutajwa jina alisema wao kamwe hawawezi kuthubutu kuharibu jina la kampuni na bidhaa zao kwa nia ovu ya kupata faida.

“Sisi ni wazalishaji wakubwa na tunaaminika ndani na nje ya Tanzania, hatuwezi kuzalisha sukari na kuiweka mchanga, tuna njia nyingi za kisasa za kubaini ubora wa bidhaa kabla ya kuwafikia walaji, hatuwezi kuingiza sokoni sukari yenye mchanga ama kitu chochote chenye kuhatarisha afya za wateja wetu,” aliongeza.

Inaendelea Uk. 13

# MO Sugar, Kagera...

Inatoka Uk. 12

### MO Sugar

Kampuni ya Mo Enterprises Limided (MeTL) ambayo inasambaza sukari yenye chapa ya MO Brown Sugar, kupitia msemaji wake, Bahati Thambikeni ililieleza Pambazuko kuwa haihusiki na sukari inayolalamikiwa kuwa na mchanga iliyopo sokoni.

"Asante kwa simu yako ukiwa unatafuta kupata ufafanuzi kutoka upande wa Mohammed Enterprises Limited kuhusiana na madai ya kuwepo sukari yenye mchanga nchini, baada ya mazungumzo yetu, nimewasiliana na mamlaka husika ndani ya kampuni…"

"Sukari iliyobainika kuwa na mchanga haikuwa ya kampuni yetu. Ilikuwa ni ya kampuni nyingine, na bidhaa hiyo tayari ilishafungiwa kuuzwa. Mamlaka husika, ikiwemo Tanzania Bureau of Standards (TBS) na Bodi ya Sukari, zinafahamu suala hilo..."

"Kwa upande wa sukari yetu ya Mo Sugar, hatujawahi kuitwa wala kuhojiwa na TBS au Bodi ya Sukari kuhusu uwepo wa mchanga au changamoto yoyote ya ubora…"

"Hadi sasa, hatujawahi kupokea mawasiliano yoyote kutoka kwa mamlaka hizo yenye ushahidi wa madai haya au taarifa yoyote inayoonyesha kuwepo kwa tatizo lolote linalohusu sukari yetu," alisema.

Alisisitiza kuwa sukari inayouzwa na kampuni hiyo inakuwa na vibali vyote kwa mujibu wa sheria zilizowekwa pia inakuwa imeidhinishwa na mamlaka zote zinazohusika.

Mmoja wa wananchi ambaye hakupenda jina lake litajwe gazetini kwa sababu za kiusalama, alisema suala hili linashtua na inaonekana serikali imekuwa ikitumia nguvu kubwa na rasilimali nyingi kulinda usalama wa wananchi wake katika baadhi ya maeneo na kujisahau hatika maeneo mengine.

"Linakuja suala kama hili la sukari ambalo ni nyeti sana kwa usalama na afya za wananchi, lakini unakuta sukari tayari inaingia na kusambazwa kwa walaji ikiwa na mchanga, ni suala la kustaajabisha kama kweli wanamaanisha kile wanachokieleza hawa serikali kuhusu kulinda usalama wa wananchi.

"Ni afadhali kwamba hadi sasa kilichobainika ni kwamba sukari ina mchanga, angalau watu wanaweza kuamini kwamba bado wako salama, hatujui mengine zaidi yaliyojificha humo, maana kama kuna kemikali nyingine zinaweza kuingia kiurahisi, usalama huu unatia shaka," alisema.

Alisisitiza kuwa suala la kulinda usalama na afya za wananchi linatakiwa lipewe nguvu zaidi hasa katika hizi bidhaa ambazo ni muhimu na zina watumiaji wengi, huku ndipo nguvu za ulinzi wa usalama zinapotakiwa kuongezwa.

Katika chapisho la wiki iiliyopita, Pambazuko liliainisha malalamiko ya wananchi kuhusu uwepo wa sukari yenye viambata vya mchanga kwenye mzunguko kwa zaidi ya miezi miwili, ulioibua sintofahamu kuhusu ubora wake na hatima ya afya za walaji.

Uwepo wa sukari hiyo inayolalamikiwa kuwa na mchanga umeelezwa na watumiaji wa chai na wale wa bidhaa za ngano, ambao wamekuwa wakilalamikia mchanga katika mikate, keki, maandazi na bidhaa nyingine za ngano zinazotengenezwa kwa kutumia sukari hiyo. Pambazuko lilifanya uchunguzi kuhusu tatizo hilo, ambapo wengi waliofikiwa na gazeti hili walionya kuwa uwepo wa bidhaa sokoni kunadhihirisha kuyumba kwa vyombo vya udhibiti wa ubora, hivyo kuhatarisha maisha ya watumiaji.

### Malalamiko

Malalamiko hayo yalithibitishwa na baadhi ya watengenezaji wa bidhaa za ngano ambao walieleza kuwa wamekuwa wakipata malalamiko kutoka kwa wateja kuhusu bidhaa zao ikiwemo mikate na maandazi kuwa na mchanga suala ambalo limekuwa likitatiza biashara zao.

Ufuatiliaji walioufanya wafanyabiashara hao walibaini kuwa mchanga huo unaolalamikiwa unatokana na matumizi ya sukari kutoka nje iliyosambaa kwenye maduka kutokana

Inaendelea Uk. 14

# MO Sugar, Kagera...

Inatoka Uk. 13

na viwanda vya ndani kusimamisha uzalishaji, ambayo ndiyo inayodaiwa kuwa na mchanga.

**Bodi ya Sukari**

Pambazuko lilizungumza na mmoja wa maofisa wa Bodi ya Sukari ambaye alieleza kuwa yeye siyo msemaji, ila akaeleza kuwepo kwa malalamiko rasmi ofisini kwao kuhusu uwepo wa sukari hiyo madukani na wanaendelea kufanya uchunguzi wao.

Pambazuko lilimtafuta Mkurugenzi wa Bodi ya Sukari, Prof. Kenneth Bengesi (pichani), na kumuuliza kuhusu malalamiko hayo, lakini akasema hawezi kuzungumzia suala hilo la kuwepo mchanga kwenye sukari kwa kuwa anayeshughulika na ubora wa sukari yupo na ndiye anayetakiwa kujibu hilo.

Alisema yeye anahusika na masuala ya utoaji wa vibali vya uingizaji wa sukari, uagizaji na uhakiki iwapo kiasi walichoagiza kimefika au la.

"Mimi suala ninaloweza kulizungumzia ni hasa iwapo vibali vimetolewa vingapi na ni akina nani waliopewa vibali hivyo, kiasi cha sukari tulichoagiza na iwapo kimeingia kwa wakati, kama hakijaingia na kama kuna uhaba wa sukari hayo ndiyo mambo ambayo ninaweza kuzungumzia..."

"Kimsingi, kuna wanaohusika na suala la ubora ndio wanaopaswa kuzungumzia suala hilo, kwa sababu ndio wanaofanya ukaguzi wa ubora wa sukari..."



"Wapo pia wanaohusika na kukagua masuala ya mionzi na mengine," alisema.

**Kauli ya TBS**

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwango Tanzania (TBS), Dkt. Ashura Katunzi, alilieleza Pambazuko kuwa ni kweli wamepata taarifa ya kuwepo kwa sukari hiyo yenye mchanga kwenye mzunguko wa bidhaa hiyo na tayari walishachukua hatua za awali za ufuatiliaji.

"Kama sehemu ya majukumu ya shirika na kwa kuzingatia misingi ya udhibiti ubora, shirika lilichukua hatua baada ya kupata taarifa ya malalamiko ya uwepo wa sukari iliyodaiwa kuwa na mchanga, ambapo ilifanya ukaguzi katika soko na kwenye maghala ya kuhifadhia sukari nchini..."

"Pia sisi hufanya uchunguzi wa kimaabara na kuweza kuzuia na kuondoa kwenye soko sukari iliyobainika kuwa na hitilafu," alieleza.

Hata hivyo, kiongozi huyo aligoma kuzitaja kampuni ambazo zimeingiza sukari hiyo, akieleza kuwa shirika hutoa huduma kwa mujibu wa matakwa ya sheria, kanuni na viwango ambapo mojawapo matakwa hayo ni kutunza taarifa za wateja (confidentiality).

Alisema utunzaji wa taarifa unaendana na misingi ya udhibiti ubora na biashara duniani, kwa taasisi inayosimamia ithibati za umahiri za kimataifa na kwamba bado wanaendelea kushughulika na kampuni hizo kiofisi.

Mkurugenzi huyo alisema TBS inaendelea kuimarisha udhibiti wa sukari inayozalishwa nchini na inayotoka nje ya nchi kupitia mifumo yake ya ukaguzi wa viwanda na maeneo ya uuzaji, uhifadhi na usambazaji, usajili wa maeneo ya uhifadhi, uthibitishaji ubora.

Pia, akasema uchunguzi wa kimaabara, ukaguzi wa sukari inayoingia nchini na ufuatiliaji katika soko ili kuhakikisha kuwa bidhaa katika soko zinakidhi matakwa ya viwango na kuendelea kulinda afya ya walaji. Aidha, alisema TBS inaendelea kuhakikisha bidhaa za sukari zilizopo sokoni ni salama kwa matumizi, akiwataka wanaotilia shaka sukari kwenye soko,watoe taarifa kupitia simu ya bure namba 0800110827.

# TPI yahimiza kuchangia vifaa kwa wenye ulemavu



**Na Mwandishi WETU**

WATAALAMU na maofisa wa tiba-mazoezi na viungo bandia Tanzania wameomba Watanzania kuchangia upatikanaji wa vifaa kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Kupitia umoja wao; Tanzania Physiotherapy Initiative (TPI), wataalamu hao wamehimiza wadau kushiriki kikamilifu katika kampeni maalumu ya kitaifa kwa ajili ya kusaidia kupata vifaa hivyo ili kurejesha tumaini kwa walemavu, hasa wa viungo.

Mwito huo upo katika taarifa ya TPI iliyotolewa wakati wa uzinduzi wa kampeni maalumu iliyopewa jina la "Move for Disability 2026" ikiwa ni harakati maalumu ya kusaidia watu wenye ulemavu nchini jijini Dar es Salaam.

Mratibu wa TPI, Estom Uvambe amesema kuelekea hitimiisho linalotarajiwa kufanyika Jumamosi ya Agosti 29, 2026, lengo hasa ni kupata vifaa vya kusaidia watu wenye ulemavu.

Akizungumza hivi karibuni, Uvambe amesema kuwa malengo ya msingi ya kampeni hiyo yenye kaulimbiu isemayo "Inclusion by Design" ni kukusanya angalau miguu bandia zaidi ya 50, viti mwendo (Wheelchairs) zaidi ya 100, fimbo nyeupe za wasioona zaidi ya 200, magongo na fimbo za kutembelea zaidi ya 300.

"Kwa hiyo tunatoa mwito kwa wadau wote, serikali na sekta binafsi tukiwaomba muendelee kuimarisha sera jumuishi na kudhamini kampeni hii ili kuleta mabadiliko ya kudumu…"

"Kwa kila Mtanzania, uhitaji kuwa tajiri ili kubadilisha maisha ya mtu, ushiriki wako, mchango wako, au hata sauti yako inaweza kuwa sababu ya mtu mwingine kupata utu na matumaini mapya…"

"Kwa vyombo vya habari, ninyi ni mabalozi wa mabadiliko. Tunaomba mtumie kalamu na majukwaa yenu kufikisha sauti hii kwa jamii nzima ili sote kwa pamoja tushirikiane kujenga Tanzania jumuishi," ameeleza Uvambe wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Ameeleza kuwa kampeni hiyo siyo ya hisani tu, bali ni harakati ya kitaifa inayolenga kuvunja vikwazo na kuleta ujumuishi wa kweli kwa ndugu wenye ulemavu nchini Tanzania ikilenga kujenga mazingira jumuishi.

"Katika jamii yetu, maelfu ya watu wanaoishi na ulemavu wa viungo au wa kuona wanakabiliwa na changamoto kubwa ya kukosa vifaa usaidizi. Kwa familia nyingi, kupata kiti mwendo, mguu bandia, magongo, au fimbo nyeupe ni mtihani mkubwa kwa sababu ya gharama…"

"Kukosekana kwa vifaa hivi kunawanyima watoto haki ya kwenda shule, kunawazuia vijana kupata ajira, na mwisho wa siku kunapunguza cheo na utu wao. Vifaa hivi siyo anasa, ni nyenzo muhimu za kurejesha matumaini na maisha ya kujitegemea," ameeleza Uvambe.

Amesema tukio hilo la kihistoria la Jumamosi Agosti 29, 2026 jijini Dar es Salaam, litawakutanisha zaidi ya washiriki 2,000 likiwajumuisha watu wenye ulemavu, wataalamu wa afya, wanamichezo, mashirika ya maendeleo, na wananchi wa kawaida kwa nia ya kutatua changamoto hiyo inayoikabili jamii.

Habari

# Kamanda Tibaigana awatonya wastaafu



*Kamishna wa Polisi Mstaafu Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Alfred Tibaigana, akiwa na Mhariri Msanifu wa Gazeti la Pambazuko, Arodia Peter wakati wa mahojiano maalum yaliyofanyika nyumbani kwake Muleba mkoani Kagera hivi karibuni. (Picha na Mpigapicha Maalum).*

Na Mwandishi WETU

KAMANDA (mstaafu) wa Jeshi la Polisi, Kanda maalum ya Dar es Salaam, Alfred Tibaigana, amewashauri watumishi wanaostaafu kuacha kukaa kwenye miji mikubwa, badala yake wakaishi kwenye miji midogo au vijijini.

Amesema uamuzi wa wastaafu kwenda kuishi maeneo ya pembezoni kutawasaidia kuendesha maisha yao kwa utulivu zaidi.

Pia anasema kufikia hatua ya kustaafu kwa mujibu wa sheria ni majaliwa ya Mungu, kwani kuna kustaafishwa au kufariki dunia kabla ya kufika mwisho, hivyo anawasihi watumishi ambao bado wako kazini kuondoa dhana na imani iliyojengeka kwamba unapostaafu vijijini hapafai.

Ameshauri kuwa mstaafu kama hana sababu kubwa za kibiashara au uwekezaji unaomfanya kuendelea kuishi kwenye majiji na miji mikubwa, basi achague kwenda kuishi maeneo yasiyokuwa na misukosuko mingi ambayo ni kwenye miji midogo au vijijini walikozaliwa.

Katika mahojiano maalum na Gazeti la Pambazuko kijijini kwake Buganguzi wilayani Muleba, Kagera hivi karibuni, Kamanda Tibaigana amesema endapo angeendelea kuishi Dar es Salaam, asingekuwa kama alivyo, kwani huko aliko ameendelea kupata watu wengi wa kuchangamana nao jambo ambalo limemsaidia kutokuwa mpweke.

"Ni bahati mbaya tumekuzwa kwamba kijijini maisha ni mabaya, magumu, lakini sisi tuliostaafu na kuamua kurudi kijijini, najihisi kama ninaishi maisha mazuri zaidi kuliko ningebakia mjini. Kwa sababu kwanza hapa nina idadi kubwa ya ndugu na marafiki tuliosoma na kucheza nao ambao hawakuajiriwa mijini, wako vijijini…"

"Hivyo najisikia mimi siyo mpweke, tofauti kama ningestaafu na kuendelea kukaa Dar es Salaam nisingeyapata haya kutokana na asili ya mji huo, watu wako busy na shughuli zao, hivyo wale watu tuliokuwa tunachangamana nao kazini nisingewaona…"

"Vilevile mimi ninaendesha shughuli zangu za kilimo na mifugo, kwa hiyo zinanipa muda wa kujishughulisha na kushughulisha mwili," anasema Kamanda Tibaigana.

**Amewekeza nini kijijini?**

Kamanda huyo mstaafu ambaye anaonekana kunawiri zaidi kwa sasa kuliko alipokuwa kazini Dar es Salaam, anasema uwekezaji wake umejikita katika kilimo ambapo anamiliki zaidi ya hekari 15 za migomba, maalum kwa uzalishaji wa ndizi za aina tofauti huku pia akiwa na hekari 20 za kahawa.

"Ninalima migomba ambapo kuna ndizi za chakula na zile za biashara tu zinaitwa Fia, katika mazingira yetu hizo haziliwi kama chakula, isipokuwa soko la nje ya Mkoa wa Kagera, zaidi mikoa ya Mwanza na kwingineko," anasema.

Yafuatayo ni sehemu ya mahojiano na Kamanda Tibaigana.

Inaendelea Uk. 17

# Kamanda Tibaigana awatonya wastaafu

Inatoka Uk. 16

**Swali:** Unadhani mtumishi anapaswa kujiandaaje kabla ya kustaafu?

**Jibu:** Kabla ya kustaafu mtumishi anapaswa kujiandaa kisaikolojia. Ajue na ajiweke tayari na kuamua kwamba baada ya kustaafu akae miji mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Mbeya nakadhalika, hii ina heka heka zake.

Pia miji ya kati kwa mfano Bukoba, Musoma, Kigoma ina utofauti wa hekaheka zake, tofauti na miji mikubwa.

Sasa aamue kama anaweza kukaa vijijini, au miji midogo ambako hakuna hekaheka ambazo mstaafu haziwezi. Anaweza kuamua kuendesha baiskeli yake, kutembea kwa miguu, ambako hakuna hekaheka kama kwenye miji mikubwa ya kupishana na bodaboda, magari makubwa na misukosuko ya hapa na pale.

**Swali:** Kwa muda uliokaa nje ya utumishi, unayaonaje mazingira ya uwekezaji huku kijijini?

**Jibu:** Kuwekeza ni suala la kisaikolojia vilevile. Kwa sababu moja kwamba wastaafu wengi wanafikiri kuwekeza ni lazima uwe na pesa taslimu.

Ukimwambia kuna kilimo na ufugaji anakwambia vinahitaji pesa, kwa hiyo kisaikolojia anadhani kila kitu hakiwezi.

Lakini ukweli ni kwamba vijiji kama hivi vya kwetu (Buganguzi) kahawa sasa hivi ipo kwenye pick, wastaafu, watu wazima na vijana wanakimbilia kulima kahawa.

Kwa mfano ukiwa na heka zako tatu hadi nne za kahawa, licha kwamba tunatumia maji ya mwenyezi Mungu, lakini mzunguko wa pesa upo. Sasa kama kama kingekuwa ni kilimo cha umwagiliaji tungekuwa na uhakika zaidi wa mzunguko wa fedha.

Kwa ujumla mtu anayetunza shamba lake vizuri huku kijijini, hata ndizi zina soko sana mapato yanakuwa mazuri zaidi na uhakika wa mzunguko wa fedha upo.

**Uchumi**

Aidha, Kamanda Tibaigana anasema suala la uchumi huko kijijini kwake inategemea na muktadha wa anayeuangalia.

“Kwa upande wangu naona siyo mzuri wala mbaya sana, jambo la muhimu ni kwamba watu wengi wanajitosheleza kwa chakula, hata kuuza ziada yakiwamo magimbi, ndizi, wanapasua mbao na magogo ya kupeleka migodini, hivyo kijiji kinachangamka.

“Na ukipita humu vijijini unaona watu wamejenga nyumba nzuri, unaona kabisa hapa kuna maendeleo, lakini ukisema tuchangie kitu fulani cha maendeleo, kila mtu anakwambia hana ela, kwa hiyo suala la uchumi inategemea mtu anavyoliangalia,” anabainisha.

**Ratiba yake ya siku**

Kamanda Tibaigana ameeleza kuwa ratiba yake ya siku inaanzia kwenye nyumba ya ibada, ambapo kila siku saa 12 asubuhi anahudhuria ibada kwenye Kanisa Katoliki lililopo kijijini kwake Buganguzi na baadaye anaendelea na shughuli nyingine za kilimo na ufugaji.

Mahojiano haya yataendelea wiki ijayo, ambapo Kamanda Tibaigana ambaye kitaaluma ni mwanasheria, anazungumzia mambo mbalimbali ya utumishi wa Jeshi la Polisi ikiwemo taratibu, kanuni na sheria zinazoongoza taasisi hiyo.



Biashara

# Dhahabu, utalii, usafirishaji vyatunisha fuko la dola

Na Mwandishi WETU

MAUZO ya nje nchini yameendelea kuimarika kupitia mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani, utalii na huduma za usafirishaji.

Sekta hizo zimefanya vizuri katika uchumi kwa mujibu wa taarifa ya mapitio ya hali ya uchumi kila mwezi inayochapishwa na Benki Kuu (BoT).

Mapitio ya uchumi kwa mwezi Mei, ambayo taarifa yake imechapishwa mwezi huu inaonyesha kuwa sekta hizo zimefanya vizuri na kuisaidia nchi kuhimili shinikizo la ongezeko la gharama za kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje zinazochochewa na changamoto za kijiografia na kisiasa duniani (geopolitics).

Taarifa ya Mapitio ya Uchumi ya Mwezi (Monthly Economic Review – MER) ya BoT inaonyesha kuwa, licha ya nakisi ya urari wa biashara kuongezeka kwa kiwango kidogo, msingi wa sekta ya nje umeendelea kuwa imara kutokana na ukuaji wa mauzo ya nje na ongezeko la mapato ya fedha za kigeni.

Katika mwaka ulioishia Mei 2026, mapitio hayo yanaonesha kuwa nakisi ya mauzo ilifikia dola za Marekani bilioni 2.21, kulinganisha na dola bilioni 2.09 iliyorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2025.

Kwa mujibu wa BoT, ongezeko hilo lilitokana zaidi na kasi kubwa ya ukuaji wa uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ikilinganishwa na mauzo ya nje.

Gharama kubwa za usafirishaji wa mizigo pamoja na bei za bidhaa katika soko la dunia zilizoendelea kuwa juu, hasa kutokana na migogoro ya Mashariki ya Kati na changamoto katika njia za usafirishaji baharini, ziliongeza gharama za uagizaji nchini.

Hata hivyo, hali hiyo haikuyumbisha kwa kiasi kikubwa nafasi ya Tanzania katika uchumi wa nje, BoT inaeleza.

Moja ya viashiria vikubwa vya uimara huo ni ongezeko la akiba ya fedha za kigeni ambayo ilifikia dola za Marekani bilioni 5.54 mwishoni mwa Mei 2026, kutoka dola bilioni 5.14 mwaka mmoja uliopita.

Kiasi hicho kilitosha kugharamia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa takribani miezi 4.3, kiwango ambacho kiko juu ya kiwango cha chini kinachokubalika kitaifa.

BoT imeeleza kuwa ongezeko hilo lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na ukuaji wa mapato yatokanayo na mauzo ya nje, hasa dhahabu, pamoja na utekelezaji wa mpango wa ununuzi wa dhahabu ndani ya nchi.

### Mauzo ya nje yapaa

Moja ya ishara kubwa ya mabadiliko chanya katika uchumi wa nje wa Tanzania ni kasi ya ukuaji wa mauzo ya nje.

Thamani ya jumla ya mauzo ya nje ya bidhaa na huduma iliongezeka kwa asilimia 17.8 na kufikia dola za Marekani bilioni 19.68 katika mwaka ulioishia Mei 2026, kutoka dola bilioni 16.71 katika kipindi kama hicho mwaka 2025.

Mauzo ya bidhaa pekee yaliongezeka kwa asilimia 20.4 na kufikia dola bilioni 11.63, jambo linaloonyesha kuwa Tanzania inaanza kuwa na vyanzo vingi vya mapato ya fedha za kigeni badala ya kutegemea bidhaa moja au chache.

Dhahabu iliendelea kuwa chanzo kikubwa zaidi cha fedha za kigeni, ambapo mapato yake yaliongezeka kwa asilimia 46.7 na kufikia dola bilioni 5.53.

Ukuaji huo ulisababishwa na ongezeko la bei ya dhahabu katika soko la kimataifa pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani.

Mbali na dhahabu, mauzo ya bidhaa za viwandani yaliongezeka kwa kasi kubwa, yakifikia dola bilioni 2.01 baada ya kukua kwa asilimia 38.3.

Ukuaji huo ulisukumwa zaidi na ongezeko la mahitaji katika masoko ya kikanda kwa bidhaa kama chuma, bidhaa za chuma na vioo.

Inaendelea Uk. 19

# Dhahabu, utalii...

Inatoka Uk. 18

Wakati huo huo, bidhaa za jadi za biashara ya nje nazo zilifanya vizuri. Mauzo ya tumbaku, kahawa na pamba yalionyesha ongezeko, yakithibitisha kuwa sekta za jadi bado zina nafasi muhimu katika uchumi wa nje wa nchi.

Takwimu hizi zinaonyesha kuwa ajenda ya Tanzania ya kuendeleza uchumi wa viwanda inaanza kuzaa matunda, huku bidhaa zinazozalishwa viwandani zikichukua nafasi kubwa zaidi katika mapato ya mauzo ya nje.

### Huduma nguzo mpya

Pamoja na mafanikio ya bidhaa, mwelekeo muhimu zaidi unaonekana katika ukuaji wa sekta ya huduma.

Mapato yatokanayo na huduma yaliongezeka kwa asilimia 14.2 na kufikia dola bilioni 8.05, yakichangiwa zaidi na utalii na usafirishaji.

Sekta ya utalii iliendelea kurejesha nafasi yake kama chanzo muhimu cha fedha za kigeni.

Mapato ya safari (travel receipts) yalifikia dola bilioni 4.42, yakisaidiwa na ongezeko la asilimia 5.9 la watalii wa kimataifa waliotembelea Tanzania ambao walifikia takribani milioni 2.3.

Mbali na utalii, sekta ya usafirishaji imeendelea kuwa injini muhimu ya ukuaji.

Mapato yatokanayo na huduma za usafirishaji yaliongezeka kwa asilimia 16 na kufikia dola bilioni 3.15.

Ukuaji huo umechangiwa na ongezeko la mizigo ya usafirishaji wa nchi jirani zinazotumia bandari na njia za Tanzania.

Hali hiyo inaonyesha umuhimu unaoongezeka wa bandari, barabara na miradi ya reli katika kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafirishaji wa kikanda, hasa kwa nchi zisizo na bandari kama Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Rwanda na Burundi.

Kwa mtazamo wa utekelezaji wa Dira 2050, mwenendo huu unaonyesha kuwa uwekezaji katika miundombinu ya usafirishaji unaanza kutoa matokeo yanayozidi biashara ya ndani na kuleta mapato ya moja kwa moja katika uchumi wa nje.

### Uagizaji bidhaa, uwekezaji

Wakati mauzo ya nje yakiongezeka, uagizaji wa bidhaa kutoka nje nao uliongezeka kwa asilimia 17.8 na kufikia dola bilioni 20.41.

Ingawa ongezeko la uagizaji lilichangia kuongezeka kwa nakisi ya urari wa bisahara, muundo wa bidhaa zilizoagizwa unaonyesha picha chanya zaidi ya uchumi.

Sehemu kubwa ya ongezeko hilo ilitokana na uagizaji wa malighafi za viwandani, mashine, vifaa vya mitambo na bidhaa za kati zinazohitajika katika uzalishaji na ujenzi wa miundombinu.

Uagizaji wa mafuta yaliyosafishwa uliongezeka kwa karibu asilimia 10 na kufikia dola bilioni 2.66, hali iliyochangiwa zaidi na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia kuliko ongezeko la matumizi pekee.

Aidha, malipo ya huduma kutoka nje yaliongezeka kwa asilimia 8.3, hasa kutokana na gharama kubwa za usafirishaji wa mizigo zilizochochewa na misukosuko ya kijiografia duniani.

### Uchumi waimarika

Kwa mtazamo wa haraka, ongezeko la nakisi ya urari wa biashara inaweza kuonekana kuwa changamoto. Hata hivyo, uchambuzi mpana wa takwimu unaonyesha hali tofauti.

Tanzania inaendelea kuongeza uwezo wake wa kupata fedha za kigeni kupitia vyanzo mbalimbali; kuanzia mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani, utalii hadi huduma za usafirishaji.

Wakati huohuo, ongezeko la uagizaji kwa kiasi kikubwa linaonekana kuchochewa na mahitaji ya uwekezaji katika uzalishaji, viwanda na miundombinu, badala ya matumizi makubwa ya bidhaa za anasa. Kwa hiyo, takwimu za BoT zinaonyesha kuwa sekta ya uchumi wa nje haiko katika hali ya kudorora, bali unapitia mabadiliko ya kimuundo.

Kwa mujibu wa baadhi ya wachumi, hali hii pia inaonesha kuwa nchi inaelekea kwenye uchumi wenye vyanzo vingi vya mapato ya fedha za kigeni, unaounganishwa zaidi na biashara ya kikanda na unaotegemea zaidi uzalishaji wa ndani.

Ikiwa mwenendo huu utaendelea, wachumi hao wanabainisha, Tanzania itakuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kukabiliana na misukosuko ya uchumi wa dunia na kuendeleza ukuaji wa uchumi kupitia ushindani mkubwa wa mauzo ya nje na upanuzi wa sekta ya huduma.

Habari

# BoT: Deni la Taifa laelekea kwenye utulivu



Gavana Benki Kuu, Emmanuel Tutuba

Na Mwandishi WETU

LICHA ya mjadala unaoendelea kuhusu kasi ya Tanzania kukopa, takwimu za hivi karibuni za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) zinaonyesha kwamba mwenendo wa deni la taifa umeanza kuingia katika hatua ya utulivu.

Aidha, BoT inaeleza kuwa sehemu kubwa ya deni inaendelea kuelekezwa kwenye miradi ya maendeleo na miundombinu.

Taarifa hiyo ya BoT inaweza kushusha kidogo ule wasi wasi ambao umeelezwa na serikali yenyewe kuwa deni la taifa ni moja ya vihatarishi katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka huu wa fedha ulioanza Julai Mosi.

Hata hivyo, taarifa hiyo ya BoT inaonyesha kuongezeka kwa kiwango cha mikopo ambayo haijaanza kutumika (undisbursed loans), jambo ambalo linaibua maswali kuhusu uwezo wa serikali kutekeleza miradi inayofadhiliwa kwa mikopo hiyo.

Kwa mujibu wa ripoti ya hali ya uchumi kwa mwezi Mei 2026 (MER), jumla ya deni la taifa ilifikia dola za Marekani bilioni 51.49 mwishoni mwa mwezi huo.

Kiasi hicho ni pungufu kidogo kulinganisha na kiasi cha deni lilivyokuwa mwishoni mwa mwezi Aprili.

Ripoti hiyo ya BoT inaeleza kuwa kushuka huko kwa kiwango cha deni kulitokana na kupungua kwa deni la nje la umma pamoja na deni la ndani.

Pamoja na mabadiliko hayo, asilimia 70.8 ya deni lote la taifa bado ni deni la nje, jambo linaloonyesha kuwa Tanzania iliendelea kutegemea zaidi vyanzo vya fedha kutoka nje kuliko soko la ndani.

Hata hivyo, hali hiyo inaweza kuanza kubadilika kuanzia mwezi huu kwani kwa mujibu wa bajeti ya 2026/27 iliyopitishwa mwezi uliopita, katika mwaka huu wa fedha serikali itakopa zaidi kwenye masoko ya ndani.

Hali hiyo inatokana na kutumba kwa masoko ya fedha ya nje na kupungua kwa misaada na mikopo kutoka kwa wafadhili wa nje.

Takwimu hizo zinaonyesha kuwa hadi mwishoni mwa Mei, deni la nje lilikuwa ni dola bilioni 36.45, ambapo asilimia 81.1 ni deni la serikali na taasisi zake, huku sekta binafsi ikichangia sehemu iliyobaki.

Katika mwezi Mei pekee, Tanzania ilipokea mikopo mipya yenye thamani ya dola milioni 125.9, lakini ililipa dola milioni 189.4 kwa huduma ya deni, zikiwemo dola milioni 140 za marejesho ya msingi.

Hii inaashiria kwamba kwa mwezi huo, kiwango cha fedha kilichotumika kulipa deni kilikuwa kikubwa kuliko mikopo iliyopokelewa.

MER inaonyesha kuwa taasisi za kimataifa zinaendelea kuwa wafadhili wakubwa wa Tanzania, zikichangia asilimia 57.5 ya deni lote la nje.

Wakopeshaji wa kibiashara wanashika nafasi ya pili kwa kuwa na asilimia 36.4, huku mikopo ya nchi mbili (bilateral loans) ikibaki chini ya asilimia tano.

Inaendelea Uk. 21

# BoT: Deni la Taifa...

Inatoka Uk. 20

Hali hii inaonyesha kuwa sehemu kubwa ya mikopo ya Tanzania bado inatokana na taasisi kama Benki ya Dunia, IMF na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), ambazo kwa kawaida hutoa mikopo yenye masharti nafuu kuliko mikopo ya kibiashara.

**Mikopo iliyochelewa**

Kuna jambo la kuvutia zaidi katika MER hiyo kuhusiana na kiwango cha mikopo ambayo tayari ilishakubaliwa, lakini hadi hivi sasa haijatolewa na wahusika.

Kwa mujibu wa BoT thamani ya mikopo ya aina hiyo imeongezeka kutoka dola bilioni 5.33 katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita hadi kufikia dola bilioni 9.05 mwezi Mei 2026.

Pamoja na mambo mengine, hii inamaanisha kuwa ipo miradi mingi ya maendeleo ambayo utekelezaji wake umesimama kusubiri kutolewa kwa fedha hizi.

Hata hivyo, ripoti hiyo ya BoT haiainishi miradi ya aina hiyo.

Lakini kwa mujibu wa wachumi, miradi inapochelewa kuanza, manufaa yaliyotarajiwa kwa uchumi nayo huchewa kufikiwa.

**Matumizi ya mikopo**

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya BoT, fedha nyingi za mikopo zimeelekezwa kwenye shughuli za kusaidia bajeti na mizania ya malipo pamoja na sekta ya usafiri na mawasiliano.

Hii inaendana na uwekezaji mkubwa unaoendelea katika reli ya kisasa (SGR), bandari, barabara na miradi mingine ya kimkakati inayolenga kuongeza ushindani wa uchumi wa Tanzania katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Kwa ujumla, takwimu za Benki Kuu hazioneshi taharuki kuhusu uhimilivu wa deni la taifa, bali zinatoa tahadhari kuhuisnaa na changamoto mpya zinazoweza kujitokeza iwapo mikopo haitadhibitiwa vyema.

Kwa mujibu wa wachumi, si mbaya kwa nchi kukopa na mjadala haupaswi kuwa tu kwenye ukubwa wa deni, bali pia kwenye kasi ya utekelezaji wa miradi inayokopeshwa, uwezo wa miradi hiyo kuzalisha mapato ya kulipa mikopo, na kuhakikisha kwamba kila dola inayokopwa inaleta tija katika uchumi na hivyo maisha ya watanzania.

Wanasema kuwa katika mazingira ya ukuaji wa uchumi unaotegemea uwekezaji mkubwa wa miundombinu, kipimo cha mafanikio hakitakuwa na uhimilivu wa deni, bali thamani ya maendeleo yatakayozalishwa na deni hilo.



Habari

# Onyo la wasomi kuhusu maandamano




**Na Waandishi WETU**

TANGU kutokea kwa vurugu wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025, Tanzania imekuwa ikishuhudia mwendelezo wa hamasa ya vitisho kutoka kwa wanaharakati wanaotaka kuwepo kwa maandamano.

Wanaharakati hao, hasa wanaoishi nje ya nchi, wanadai kufanyika kwa maandamano ili kushinikiza serikali kuchukua hatua dhidi ya madai ya kukiukwa kwa haki za binadamu na kuminywa kwa demokrasia.

Kila inapotangazwa tarehe ya kufanyika kwa maandamano hayo, serikali imekuwa ikitumia vyombo vya dola kuimarisha ulinzi katika maeneo mengi, hasa ya majiji makubwa ikiwamo Dar es Salaam.

Lakini kwa ujumla, siku ambayo inatangazwa kuwa ndio maandamano hayo yatafanyika, Tanzania inakuwa kama imefungwa kwani askari wanatanda mitaani huku raia wakijifungia ndani.

Shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii zinadorora kwa kiasi kikubwa siku hiyo.

Kwa mara ya mwisho tumeshuhudia haya Julai 7, siku ya kilele cha maadhimisho ya sherehe za Sabasaba mwaka huu.

Kwa kawaida siku hii hutawaliwa na pilikapilika nyingi, hasa katika viwanja vya maonyesho ya kimataifa ya biashara katika Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam.

Lakini hali ilikuwa tofauti mwaka huu kwani siku hiyo ilikosa msisimko huku viwanja hivyo vikiwa vitupu. Watu walihofia kutoka majumbani kwa hofu ya kutokea rabdha wakati wa maandamano.

Baadhi ya watu wameanza kujiuliza; hivi nchi itaendelea katika mtindo huu wa maisha hadi lini? Hali hii ya vitisho kusababisha watu kujifungia, usalama kuongezwa na shughuli za kiuchumi na kijamii kudorora itadumu mpaka lini? Hali hiyo ina madhara gani kwa watu na kwa nchi?

Pambazuko lilijitahidi kuwatafuta wataalamu wa masuala mbalimbali ili kupata majibu ya baadhi ya maswali hayo na pia ushauri wa nini kifanyike ili kuiondoa nchi kwenye mtanziko huo.

Miongoni mwa watu ambao wamezungumza na Pambazuko ni wanasaikolojia ambao wanaonya kuwa hali hiyo inatoa ishara mbaya kwa nchi.

Ingawa hatua zinazochukuliwa na serikali kukabiliana na matishio hayo ya maandamano zinazaa matunda - kwa maana ya kufanikiwa kuzuia maandamano, lakini bado jambo hilo lina madhara makubwa, wanasema wanasaikolojia hao.

Mtaalamu wa saikolojia wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dkt. Shaghembe Magholanga, amesema tishio la maandamano ya kila mara linaleta kumbukumbu za kilichotokea Oktoba 29, 2025 ambapo watu wengi walipoteza maisha. Tanzania haikuwahi kushuhudia tukio la aina ile na kwa ukubwa ule.

Anasema hilo linawafanya baadhi ya watu kuwa katika hali ya kuvurugwa, wengine bado wana kiwewe - wanaogopa hata kupita maeneo ambayo vurugu hizo zilitokea.

Msomi huyo ameshauri kutafutwa kwa suluhu ya kudumu ili vitisho kama hivyo visiwepo tena kwani kila vinapotokea huamsha hisia tofauti kwa baadhi ya watu, jambo ambalo linaathiri afya yao ya akili.

Aidha, ameonya kuwa endapo hali hiyo ikiendelea nchi itarajie athari kadhaa, mojawapo ikiwa ni watu kushindwa kushiriki kwenye shughuli mbalimbali za kijamii na za uzalishaji mali.

Inaendelea Uk. 23

# Onyo la wasomi...

Inatoka Uk. 22

Mwanazuoni huyo anasema na kwa kadri taifa linavyochelewa kuponya majeraha hayo gharama zitakuwa kubwa ikiwamo matatizo ya afya ya akili, chuki kuenea baina ya mtu na mtu na pia taasisi kwa taasisi.

Dkt. Magholanga anasema matukio ya Oktoba 29, 2025 yameacha mpasuko, na kisaikolojia yametengeneza na kuacha chuki baina ya kundi moja dhidi ya jingine na kuna watu ambao wana chuki na serikali, hawajakubali kilichotokea.

Anasema kuna haja ya kuyaleta makundi hayo pamoja kupitia mpango mahsusi wa kuyaunganisha makundi hayo ili kuondoa ushindani wa nguvu na madaraka.

"Kwa kuwa yale maandamano ya Oktoba 29, 2025 yalitokea kwa sababu kuna madai waliyokuwa nayo, watu hao wanafikiri namna nyingine ya kuendelea kudai kile wanachokitamani ni kuendelea kudai kupitia njia hii ya maandamano ambayo wanayatangaza kupitia mitandao ya kijamii kwa sababu wanajua wakitangaza, lazima kuna kundi la watu ambalo litatoka, lakini kwa lugha nyingine hata kama watu hawatatoka, watakuwa wamefikisha ujumbe..."

"Lakini pia hizi vurugu ni viashiria vya majeraha ya kisaikolojia ambayo watu bado wanayo. Itafika hatua mtu anaona kwamba hana cha kupoteza, hivyo kama taifa tunapaswa kufanya jitihada za makusudi kuweza kuponya majeraha ya mtu mmoja mmoja, baadhi ya familia jamii na taifa kwa ujumla," ameshauri.

Mtaalam mwingine wa ustawi wa jamii, Joseph Kayinga, amesema tishio la maandamano linalotolewa mara kwa mara na kusababisha watu kushindwa kutoka majumbani ni kiashiria kwamba jamii sasa haiko sawa kulingana na kanuni za usawa.

Amesema masuala ya kijamii hayatatuliwi kwa mtutu wa bunduki bali kwa kuwatumia wataalam wa jamii ambao wana sosiolojia, atroporojia, saikolojia na ustawi wa jamii.

Kayinga amesema kinachoendelea nchini ni kuondoka kwa utengamano wa kijamii ambapo wanasiasa wameamua kutatua matatizo ya kijamii kwa kutumia mtutu wa bunduki, jambo ambalo haliwezi kusaidia kutatua tatizo lililopo kwa sababu si mahala pake.

"Watu kusikilizana katika utengamano kumeanza kuondoka, tumetoka kwenye ile kawaida, desturi haipo na panapokuwa na hali hiyo lazima turudi nyuma, kuna kitu ambacho hakiko sawa, zamani watu walikuwa hawatekwi, wanasiasa walikuwa hawafungiwi sasa wanafungiwa na wanatekwa.

"Kuna sababu za watu kutishia kuandamana, tuondoe hizo sababu ili jamii irudi kuwa sawa. Kama tumeamua kutatua matatizo ya kijamii kwa kutumia mbinu za kijeshi tujue tumefeli. Kama tunatibu matatizo ya kiafya kwa kutumia siasa tujue tumefeli. Na kama tunatibu matatizo ya kiuchumi kijeshi tujue tumefeli huku pia matatizo ya kiusalama yanapaswa kutibiwa kiusalama," anasema Kayinga.

Aidha, baadhi ya wachambuzi wanasema tishio la maandamano ya Julai 7, mwaka huu na mengine yanayotarajiwa yanalenga kudhoofisha uchumi wa nchi kwa kutumia kile kinachoitwa 'digital economic sabotage', ambapo kwa mujibu wa tafsiri isiyo rasmi ni kitendo cha kutumia mitandao ya kijamii kudhoofisha taasisi au uchumi wa serikali kwa makusudi.

Mwananchi mwingine aliyehojiwa na Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Ujerumani (DW), Innocent Kailima, anahoji; "Kweli taifa letu lina amani ya kweli? Nchi hailindwi na bunduki, hailindwi na purukushani..."

"Sasa kama tumefikia hapa, haya ni mambo ambayo hayana afya kwa watawala wala watawaliwa, kwa sababu kama raia ndiyo wanachafua amani, amani ikishaharibika mtawala hana mahali pa kuweka mguu na mtawaliwa hana mahali pa kuweka miguu..."

"Kwa hiyo ni lazima wote tujitafakari; wakati raia anadhibitiwa, watawala nao wajitafakari, je wako sahihi? Haya yanayotokea yanatokea kwa sababu gani? Ni kwa sababu ya raia au ni watawala? Lakini kubwa la kujihoji kwa pande zote ni; Je, taifa letu kweli lina amani ya kweli?"

Kwa hali jinsi ilivyo, kuna uwezekano mchezo huu wa kutishia kuandamana na serikali kujihami kwa kusambaza askari utaendelea kwani wahamasishaji hao wa maandamano wameitaja tena Agosti 8 kuwa siku nyingine ya maandamano. Hii ni siku ya kilele cha maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima nchini.



Kilinge cha Mawasiliano

Na Loth MAKUZA

# Tanzania tulikosa ushawishi kwa Dangote

KATIKA kushindwa jambo, lazima kuna sababu, iliyosababisha hatua hiyo na kuleta maumivu.

Hivi karibuni Tanzania ilikumbwa na maumivu ya kukosa fursa ya uwekezaji mkubwa uliotarajiwa kufanywa na Aliko Dangote, tajiri namba moja Afrika.

Dangote aliamua kuwekeza mabilioni ya dola huko eneo la Lamu, Kenya, kwa mradi wake wa dola bilioni 17 wa kiwanda cha kusafisha mafuta.

Niseme wazi Tanzania haikupoteza kiwanda hiki kwa sababu ya pwani au jiografia. Imepoteza, kwa kiasi kikubwa, kwa pengo la mawasiliano na ushawishi (lobbying). Kama hatutalikubali hili, tutaendelea kupoteza mikataba mingine.

Kwa miezi kadhaa, Kenya, Uganda na Tanzania walikuwa katika mashindano ya kimyakimya kuvutia uwekezaji huu mkubwa zaidi Afrika Mashariki.

Aprili, Dangote alionekana katika picha ya pamoja na Rais William Ruto wa Kenya na Yoweri Museveni wa Uganda baada ya mazungumzo ya kutangaza nia ya kujenga kiwanda cha kusafisha mafuta katika eneo la Afrika Mashariki.

Kukaendelea mawasiliano ya viongozi hao na kufikia Julai, Kenya ilishinda. Naibu Rais Kithure Kindiki ndiye alikuwa akiongoza kamati maalum ya serikali yake kushirikiana na wawekezaji, miezi kabla ya tangazo, kuiwezesha Kenya kupata uwekezaji huo.

Kenya iliahidi mtaji wa awali, benki zake zenye nguvu zilitoa uhakika wa kifedha, ikiwa ni mchango wa uwekezaji huo.



Rais Samia Suluhu Hassan alikutana na Dangote Dar es Salaam mara kadhaa, wakati vyombo vya habari vya kikanda tayari vikieleza ushindani mkali kati ya Tanga na Mombasa.

Taarifa zinaonyesha Tanzania iliingia kwenye mazungumzo rasmi kwa kuchelewa.

Kufikia wakati viongozi hao wawili walipoketi mezani, mengi tayari yalikuwa yameshapangwa upande wa Kenya.

Wataalamu wa mawasiliano tunajua jambo moja; mtaji mkubwa hauji kwa bahati. Unashawishiwa, unaratibu kila hatua, na kutumia watu ambao kazi yao ni kuondoa shaka akilini mwa mwekezaji kabla mikataba haijafika. Hiyo ni kazi ya mawasiliano na ushawishi.

Kenya ilifanya mambo matatu vizuri; sauti moja ya serikali kupitia kamati ya Kindiki, kutenga fedha, siyo kwenda na maneno matupu kwa mwekezaji na ahadi ya kulinda uwekezaji huo.

Mara nyingi sisi tunachukulia mawasiliano kama kazi ya baadaye, kuandika taarifa kwa vyombo vya habari baada ya uamuzi kufanyika, badala ya kuwepo mezani wakati uamuzi unatengenezwa.

Tunaruhusu siasa za ndani kula muda ambao ungetumika kwa fursa za nje, tunashindania mtaji kama tunavyoshindania misaada, kwa tabasamu, si miundombinu ya uaminifu.

Jinsi ya kurekebisha

Sasa basi, ni vyema tuwape wataalamu wa mawasiliano nafasi mezani kabla ya mkataba, na tujenge uwezo wa kudumu wa kufuatilia miradi mikubwa duniani mapema.

Kama Tanzania iliweza kupata mradi mkubwa wa bomba la mafuta ghafi inawezekana kabisa tulishindwa kupata uwekezaji mwngine wa Dangote kwa kushindwa ushawishi.

Kupanga ni kuchagua.

***Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@lothmakuza.co.tz***

Na Emmanuel JACOB



# Wheelchair siyo anasa, ni chombo cha ukombozi

SISI wenye uwezo wa kutembea kwa miguu miwili hatuvai viatu vya michezo (raba) kwenye sherehe za usiku, wala hatuvai viatu vya ofisi kupanda milima au kukimbia mchangani, tunabadilisha viatu kulingana na mazingira na mahitaji yetu.

Vivyo hivyo, kwa rafiki zetu ambao muda wote wanatumia viti-mwendo, maarufu kwa jina la Kiingereza; wheelchair kujongea, mara nyingi hawana uchaguzi.

Kiti mwendo kimoja hakiwezi kukabiliana na barabara zetu za mitaani zenye mashimo na kokoto, milango membamba ya ofisi, na harakati za kila siku za kijamii.

Hata hivyo, jamii yetu bado inatazama wheelchair kama kifaa cha kawaida tu cha "saizi moja inafaa wote." Ukweli ni kwamba, kiti hiki siyo samani tu ya kukalia, ni kiungo cha mwili wa binadamu, ni haki ya msingi ya afya, na ni chombo pekee cha ukombozi kinachompa mtumiaji uhuru wa kuishi maisha yake kikamilifu.

Kwa wasomaji wa gazeti la Pambazuko, ni wakati wa kuangalia suala hili tofauti na haya ni mambo muhimu ya kuzingatia kuhusu viti-mwendo kama hitaji la msingi.

Bila kiti-mwendo kilichopimwa na kurekebishwa vizuri kulingana na umbo la mtumiaji, kuna hatari kubwa ya kupata madhara hatari kama vile vidonda vitokanavyo na mgandamizo (pressure sores), maumivu makali ya mgongo, na matatizo ya muda mrefu ya viungo au uti wa mgongo.

Kiti kinachomfaa mtumiaji hupunguza kwa kiasi kikubwa uchovu na maumivu ya misuli ya mikono na mabega.

Vifaa hivi vya usafiri vinasaidia moja kwa moja kupiga vita upweke na kutengwa kijamii.

Tafiti zinaonyesha kuwa kupata kiti cha magurudumu kinachofaa kunaimarisha sana uwezo wa mtu kujitegemea.

Hali hii inawawezesha watumiaji kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii na kiuchumi, ikiwemo kuingia katika soko la ajira na kuchangia maendeleo.

Kila mtumiaji ana mahitaji ya kipekee; hivyo basi, kurekebisha kiti kulingana na hitaji la mtu siyo jambo la ziada, bali ni lazima.

Wakati viti vizito na vya kawaida (depot chairs) vinafaa kwa matumizi ya muda mfupi kama vile kusafirishia wagonjwa hospitalini, watumiaji wa kila siku wanaofanya kazi wanahitaji viti vyepesi.

Lakini pia, wanahitaji sehemu maalum za kuegemea mgongo ili kulinda miili yao dhidi ya majeraha ya muda mrefu.

Ukweli ni kwamba, mchakato wa kutafuta kiti sahihi unaweza kuwa mgumu na wenye changamoto nyingi kutokana na gharama kubwa za vifaa hivi.

Aidha, mifumo ya bima ya afya mara nyingine haihusishi. Ili kuelewa hasa kiti wheelchair, au kubadilisha mara inapohitajika. Wengi wetu hawazingatii ni kiti gani kinamfaa mgonjwa au mtumiaji wa muda mrefu.

Hivyo, ni muhimu kushirikiana na wataalamu wa tiba viungo (physiotherapists) na utengamao ambao wanaweza kupima mahitaji halisi ya mwili wa mtu.

*__Mwandishi Emmanuel Jacob ni Afisa Mfiziotherapia (Ameandika Kitabu cha Mbinu za Kutibu Maumivu Sugu). Simu: 0765359305 Instagram: Emmanuel Jacob__*



Bustani ya Sheria



Na Karim Gabriel Mussa

# Korti yaweka wazi mipaka ya Bakwata

DESEMBA 24, 2025, Mahakama Kuu ya Tanzania, Masijala ya Dar es Salaam, ilitoa uamuzi muhimu katika shauri la Sheikh Prof. Hamza Mustafa Njozi & Others v. Registrar of Societies & Others [2025] TZHC 8595, ukigusa uhuru wa dini na uwakilishi wa taasisi za Kiislamu.

Miongoni mwa hoja zilizojitokeza ilikuwa iwapo Bakwata inaweza kuchukuliwa kuwa mwakilishi wa Waislamu wote nchini na mipaka ya mamlaka ya serikali katika masuala ya taasisi za dini.

Mahakama ilisisitiza kuwa hakuna taasisi ya dini iliyo juu ya Katiba au sheria, na kwamba haki ya uhuru wa dini inayolindwa na Ibara ya 19 ya Katiba inapaswa kuheshimiwa. Aidha, ilieleza kuwa mamlaka ya serikali yanapaswa kutekelezwa kwa kuzingatia sheria na misingi ya haki za kikatiba.

Kuhusu Bakwata, Mahakama ilirejea Katiba ya taasisi hiyo na kubainisha kuwa inaeleza uwakilishi wake kwa mujibu wa malengo na muundo wake.

Kwa msingi huo, Mahakama haikukubaliana na hoja kwamba Bakwata ni mwakilishi wa madhehebu yote ya Kiislamu nchini.

Uamuzi huo unaonyesha kuwa taasisi nyingine za Kiislamu zinaweza kuwepo na kujiendesha kwa mujibu wa sheria na Katiba bila kulazimika kuwa chini ya Bakwata, mradi zinatimiza masharti ya kisheria yanayosimamia usajili na uendeshaji wa jumuiya za dini.

Kesi hii imekuwa rejea muhimu katika kufafanua kuwa uhuru wa dini unajumuisha haki ya taasisi za kidini kujiendesha kwa mujibu wa imani na taratibu zao, huku zikiheshimu sheria za nchi.

Pia inasisitiza kuwa uwakilishi wa taasisi moja haupaswi kudhaniwa kuhusisha makundi yote ya waumini bila msingi wa kisheria.

Kwa hiyo, uamuzi huu unaimarisha kanuni kwamba katika Tanzania yenye mfumo wa kidemokrasia na utawala wa sheria, hakuna taasisi ya dini inayoweza kudai mamlaka juu ya madhehebu mengine isipokuwa pale ambapo mamlaka hayo yametolewa na sheria au yamekubaliwa na wahusika wenyewe.

Hivyo, uhuru wa dini na usawa wa taasisi za kidini vinaendelea kuwa miongoni mwa nguzo muhimu za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



***Mwandishi ni Mwanasheria na Mchambuzi wa Sheria kutoka KGM Attorneys). Anapatikana kwa namba: 0755 395 572 au Email: karimbinmussa@gmail.com***



Na Rashid MTAGALUKA

## Hoja Yangu

# Chondechonde viongozi wa dini

MITANDAO ya kijamii imekuwa sehemu muhimu ya maisha ya Watanzania. Mbali na kurahisisha mawasiliano, imegeuka kuwa jukwaa la mijadala ya dini, siasa na masuala ya kijamii.

Hata hivyo, wiki iliyopita tumeshuhudia jinsi mijadala inayowahusu viongozi wa dini ilivyotawala majukwaa ya kidijitali, jambo linalozua swali muhimu; je, mitandao inajenga au inabomoa heshima ya taasisi za dini?

Kwa upande mmoja, kumekuwa na mjadala mkubwa kuhusu Sheikh Nurudeen Muhammad Ahmad (Sheikh Kishk), Mkurugenzi wa Al-Hikma Foundation, ambaye kwa miaka ya hivi karibuni amejijengea ushawishi mkubwa kupitia mihadhara, mashindano ya Qur'an na matumizi ya majukwaa ya kidijitali kufikisha ujumbe wa dini kwa maelfu ya watu.

Umaarufu wake unaonyesha namna teknolojia ilivyopanua wigo wa dawah na kuwafikia vijana wengi.

Kwa upande mwingine, mitandao ilifurika taarifa kuhusu mabadiliko ya uongozi ndani ya Bakwata baada ya kutangazwa kuondolewa kwa Sheikh Walid Alhad Omar Kawambwa katika nafasi ya Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam na kukaimishwa kiongozi mwingine.

Habari hizo zilisambazwa kwa kasi kubwa, zikiambatana na maoni, lawama, kejeli na hata hukumu kutoka kwa watu ambao hawakuwa na taarifa kamili kuhusu mchakato wa uamuzi.

Matukio haya mawili yanatoa funzo muhimu. Mitandao ya kijamii siyo adui wa dini, bali namna inavyotumika ndiyo inaweza kujenga au kubomoa.

Kiongozi wa dini anapokuwa mfano wa maadili na busara, mitandao huwa daraja la kueneza elimu, lakini inapogeuzwa uwanja wa matusi, uzushi na hukumu za haraka, madhara yake huikumba jamii nzima.

Uislamu umeweka misingi ya kuthibitisha habari kabla ya kuzisambaza. Katika zama za kidijitali, maadili hayo yanapaswa kuwa ngao dhidi ya taarifa zisizo na uthibitisho.

Ni rahisi leo video fupi au chapisho moja kusambaa kwa maelfu ya watu ndani ya dakika



chache, lakini athari yake kwa heshima ya mtu au taasisi inaweza kudumu kwa miaka.

Kwa viongozi wa dini, changamoto ya sasa siyo kuhubiri misikitini pekee, bali pia kuongoza mazungumzo yenye staha kwenye majukwaa ya kidijitali. Kwa waumini, wajibu si kushabikia kila taarifa, bali kuchuja, kuthibitisha na kujadili kwa heshima. Tofauti za maoni hazipaswi kugeuzwa sababu ya matusi au kugawanya umma.

Tanzania imejengwa juu ya misingi ya amani na kuvumiliana. Misingi hiyo inaweza kudhoofishwa endapo mitandao ya kijamii itaendelea kutumiwa kama mahakama ya kutoa hukumu bila ushahidi.

Taasisi za dini nazo zinapaswa kuendelea kuwasiliana kwa uwazi ili kupunguza nafasi ya uvumi na tafsiri zinazoweza kupotosha.

Kwa hiyo, somo la wiki hii siyo kuhusu Sheikh Kishk au Sheikh Walid pekee, ni kuhusu namna jamii yetu inavyotumia teknolojia.


Mitandao ya kijamii inaweza kuwa chombo cha kueneza elimu, kuimarisha maadili na kujenga umoja, au ikawa chanzo cha migawanyiko na kuporomoka kwa heshima ya viongozi na taasisi. Chaguo lipo mikononi mwa watumiaji wake.

Tanzania inahitaji uhuru wa kujieleza unaoambatana na uwajibikaji, heshima na ukweli na hapo ndipo teknolojia itakapokuwa baraka badala ya kuwa chanzo cha migogoro.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com***

## Nionavyo

# Tusimchukie Dangote, anafungulia mlango mpya wa nishati




**Na Peter NYANJE**

UAMUZI wa bilionea wa Nigeria, Aliko Dangote, kujenga kiwanda kikubwa cha kusafisha mafuta ghafi katika kisiwa cha Lamu nchini Kenya, unaweza kuwa moja ya matukio muhimu zaidi katika historia ya sekta ya nishati Afrika Mashariki.

Tanzania inaweza kuwa hivi sasa inajilaumu kwa kuukosa mradi huu mkubwa, lakini haipaswi kujilaumu sana kwani bado ina nafasi ya kunufaika licha ya kuwa uwekezaji huu mkubwa unafanyika nchi jirani.

Ingawa mradi huo utawekezwa nchini Kenya, athari zake za kiuchumi zinatarajiwa kuvuka mipaka na kuigusa Tanzania kwa namna ambayo inaweza kubadili mwelekeo wa kiuchumi kupitia usalama wa nishati, gharama za uzalishaji na ushindani wa viwanda kwa miaka mingi ijayo.

Kiwanda hicho kinatarajiwa kusafisha mapipa 700,000 ya mafuta kwa siku, kiwango kitakachokifanya kuwa cha pili kwa ukubwa Afrika baada ya kiwanda cha Dangote kilichopo Lagos nchini Nigeria.

Kwa makadirio ya gharama za uwekezaji ya hadi dola za Marekani bilioni 17, mradi huo ni miongoni mwa uwekezaji mkubwa zaidi wa sekta binafsi kuwahi kufanyika Afrika Mashariki.

Kwa sasa, Tanzania na nchi nyingi za ukanda huu hutegemea mafuta yaliyosafishwa kutoka Mashariki ya Kati, India na Asia.

Hali hiyo imekuwa ikiweka uchumi wa eneo hili katika hatari ya misukosuko ya kimataifa, kama vile ambavyo tunashuhudia hivi sasa kutokana na vita baina ya Iran dhidi ya Marekani na Israel.

Kuanzia janga la Covid -19, vita vya Russia na Ukraine hadi mvutano unaoendelea Mashariki ya Kati, kila mshtuko wa kimataifa umekuwa ukisababisha ongezeko la bei za mafuta na gharama za usafirishaji, hali inayochochea mfumuko wa bei na kuongeza gharama za uzalishaji hapa nchini.

Kwa upande wa Tanzania, ingawa baadhi ya watu wameshaanza kuona kuwa Tanzania imepoteza, lakini manufaa ya uwekezaji wa kiwanda cha Lamu yanaweza kuwa makubwa kuliko inavyoweza kufikiriwa.

Hivi sasa Tanzania inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo reli ya kisasa (SGR), upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (Eacop), pamoja na uwekezaji mkubwa katika sekta za madini na viwanda.

Miradi yote hiyo inahitaji upatikanaji wa mafuta kwa uhakika na kwa gharama zinazoweza kutabirika. Hapa ndipo unapoanza kuona umuhimu wa uwekezaji huu kwa Tanzania.

Wachumi wamekuwa wakisisitiza mara kwa mara kuwa gharama za nishati ni miongoni mwa sababu zinazopunguza ushindani wa viwanda vya Afrika Mashariki dhidi ya bidhaa kutoka Asia.

Inaendelea Uk. 29

# Tusimchukie Dangote

Inatoka Uk. 28

Kwa mtazamo huo, kuwepo kwa kiwanda kikubwa cha kusafisha mafuta ndani ya ukanda huu kunaweza kusaidia kupunguza gharama za usafirishaji wa mafuta na kuongeza uhakika wa upatikanaji wake.

Takwimu za Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) zinaonesha kuwa gharama za usafirishaji na nishati ni miongoni mwa vikwazo vikubwa vinavyozuia kasi ya ukuaji wa viwanda barani Afrika.

Benki hiyo imekuwa ikisisitiza kuwa uwekezaji katika miundombinu ya nishati ni muhimu kwa kufanikisha ajenda ya viwanda na biashara ya kikanda.

Mradi wa Dangote pia unaibuka katika kipindi ambacho Afrika inatekeleza kwa nguvu mpango wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA).

Badala ya nchi za Afrika kuendelea kuagiza mafuta yaliyosafishwa kutoka mabara mengine, kiwanda hicho kinaweza kuwa sehemu ya mnyororo mpya wa thamani unaowezesha nchi za Afrika kunufaika zaidi na rasilimali na masoko yao wenyewe.

Kwa Tanzania, jambo la kuvutia ni kwamba kwa miezi kadhaa ilikuwa ikitajwa miongoni mwa maeneo yaliyokuwa yanawaniwa kuupokea mradi huo kabla ya Dangote kuamua kuujenga Lamu.

Ingawa Tanzania imekosa uwekezaji huo moja kwa moja, wachambuzi wanaamini bado inaweza kuwa mmoja wa wanufaika wakubwa kutokana na ukaribu wake wa kijiografia na nafasi yake kama kitovu cha usafirishaji katika ukanda huu, hasa kupitia SGR na Bandari ya Dar es Salaam ambayo imeboreshwa kwa kiasi kikubwa.

Aidha, mradi huo unaweza kuwa kichocheo kwa Tanzania kuharakisha mipango yake ya kuendeleza sekta ya mafuta na gesi, hususan miradi ya kuongeza thamani ya gesi kabla ya kuzipeleka sokoni bidhaa badala ya kuiuza gesi kama ilivyo.

Tanzania tayari ina akiba kubwa ya gesi asilia inayokadiriwa kufikia futi za ujazo trilioni 57, ambazo zinaweza kuwa msingi wa uwekezaji mkubwa wa viwanda vya nishati katika siku zijazo.

Hata hivyo, pamoja na fursa hizo, yapo maswali kuhusu athari za mazingira.

Kisiwa cha Lamu ni eneo lililotangazwa na Unesco kuwa urithi wa dunia, na wanamazingira wameonya kuhusu hatari za kurudia makosa yaliyoshuhudiwa katika Delta ya Niger nchini Nigeria, ambako shughuli za mafuta zilisababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

Lakini kwa upande wa uchumi, ujumbe unaojitokeza ni mmoja. Afrika Mashariki inaelekea katika zama mpya ambapo usalama wa nishati utaamua ushindani wa viwanda, biashara na uwekezaji.

Katika mazingira hayo, kiwanda cha Dangote kinaweza kuwa zaidi ya mradi wa kusafisha mafuta; kinaweza kuwa nguzo mpya ya mageuzi ya uchumi wa ukanda huu.

Kwa Tanzania, mafanikio ya mradi huo yanaweza kumaanisha mafuta ya bei nafuu zaidi, gharama ndogo za uzalishaji, ushindani mkubwa wa viwanda na mazingira bora ya uwekezaji.

Na katika safari ya kuelekea Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, huo unaweza kuwa mchango mkubwa kupitia mapipa 700,000 ya mafuta yatakayozalishwa kila siku.

***Mwandishi ni Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Pambazuko. Anapatikana kwa namba ya simu: 0784 211 716***



*Aliko Dangote*

# Barua za Wasomaji



**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

## Tabata tumechoka kwa mateso

**Mhariri,**
SISI wakazi wa Tabata hasa maeneo ya Tugusako, mitaa ya Bandari, Mbuyuni na Chuo cha Ualimu cha St. Marys tumekuwa katika wakati mgumu kwa muda mrefu sasa, hasa kutokana na ukosefu wa maji safi ya Dawasa.

Ni karibu miezi sita sasa, hatuna huduma ya maji na tatizo hili ni kama limeanza kuzoeleka, huku malalamiko yetu kwa Dawasa yakiwa ni kama hayasikiki, yamepuuzwa. Hakuna anayejali. Tumewasilisha malalamiko yetu kwa njia zote, kufika ofisini kwa meneja wa Dawasa Tabata, kupitia kundi sogozi la Whatsapp lililoanzishwa kwa ajili ya ufuatiliaji likijumuisha viongozi na watendaji wa Dawasa na wananchi, lakini hakuna ufumbuzi katika suala hili.

Kwa wakazi wa maeneo haya, kwa sasa hatuna uhakika wa afya zetu, akina mama wameanza kulalamika maumivu ya migongo, wakazi wengi tumejikuta kwenye msongo wa mawazo hasa kutokana na kutokuwa na uhakika wa maji kwa ajili ya shughuli za nyumbani. Malalamiko ya magonjwa ya ngozi ikiwemo ukurutu hadi sehemu za siri yanayotokana na kutokuwa na uhakika wa kuoga kwetu limeanza kuwa jambo la kawaida.

Tunaiomba serikali kupitia kwa Waziri wa Maji, Jumaa Aweso itusaidie kutunusuru katika jehanamu hii.

**James Kapaya, Mtaa wa Bandari,**

## Serikali ione aibu barabara ya Moro-Dodoma

**Mhariri,**
MARA nyingi ni msafiri wa mara kwa mara kati ya Dar es Salaam na Dodoma, lakini nakerwa na ubovu wa kipande cha barabara kati ya Morogoro na Dodoma. Ni aibu kuona njia inayoelekea makao makuu ya Tanzania ikiwa na ubovu.

Kitu cha ajabu ni kuwa serikali imekuwa ikikarabati barabara hiyo kwa vipande vidogo vidogo na kazi hiyo huchukua muda mrefu.

Kwa zaidi ya miaka mitatu sasa michepuko katika barabara hii limekuwa ni jambo la kawaida kutokana na ukarabati huo wa vipande vipande. Hivi wataalamu serikalini hawajui kuwa barabara hii ni moja ya barabara ambazo muda wake wa matumizi ulishamalizika?

Hivi serikali kweli haina fedha za kuitengeneza barabara hii kwa hadhi ya barabara inayoelekea makao makuu ya nchi?

Serikali ituondolee aibu ya barabara hii.

**Lwitiko Msafiri,**
**Kibaha Maili Moja,**

## Latra iongeze usimamizi mabasi ya usiku

**Mhariri,**
MIMI ni mmoja wa watu ambao wanafurahia sana utaratibu wa mabasi ya abiria kusafiri usiku.

Kuanzishwa kwa usafiri huu kumesaidia sana katika suala la uchumi hasa kwa watu tunaothamini muda.

Wakati usafiri huu unarejeshwa kulikuwa na wasi wasi kuwa huenda ukasababisha ajali lakini hilo halijashuhudiwa kwa sababu ya mifumo mizuri ya usimamizi.

Lakini nimeanza kupatwa na wasi wasi kuhusu usimamizi huo baada ya wiki iliyopita kushuhudia dereva ambaye alisafiri usiku na kufika Dodoma asubuhi, kuendelea na safari ya basi hilo kurudi Dar es Salaam. Nilidhani kuwa mifumo ya Latra haiwezi kumruhusu dereva aliyesafiri usiku kucha kuendelea na safari asubuhi kabla hajapata muda wa kupumzika.

Mambo kama haya yakiachwa yaendelee ipo hatari tukaanza kushuhudia mambo ya ajabu kwenye haya mabasi yanayosafiri usiku.

**Mohamed Likwata,**
**Segerea, Dar es Salaam.**


MOVE FOR DISABILITY
INCLUSION BY DESIGN 26'
WALK
with Us
29th August 2026
SPONSERED BY circleg
Kua mshiriki kwa Tshs 40,000/- Tu!
Nunua ticket yako kutumia Lipa Namba
MOVE FOR DISABILITY
6 1 2 4 6 6 1 0
INCLUSION BY DESIGN 26'
SPONSERED BY
circleg
Pambazuko

■ Wazo Binafsi

# Upungufu wa walimu upo au hila?



Na Allan LAWA, Izazi

“ELIMU ni zana adhimu, yenye nguvu, ina uwezo wa kuibadilisha jamii na ulimwengu kama itatumika kikamilifu na kwa kuzingatia misingi yake.”

Hii ni nukuu maarufu ya Nelson Mandela, kiongozi wa kwanza wa Afrika Kusini huru baada ya kuutokomeza utawala wa kibaguzi wa nchi hiyo mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Mandela aliitumia nukuu hii mara nyingi katika kushajihisha umuhimu wa elimu kwa watu wake na jamii yote duniani kwa kuitaka kuipa kipaumbele sekta ya elimu hasa kwa mataifa yanayoendelea duniani kote.

Nimeanza na nukuu ya Mandela baada ya kuwapo taarifa ya Tamisemi kuhusu Elimumsingi (BEST 2025) inayoonyesha kuwa Tanzania ina upungufu mkubwa wa walimu kwenye shule za msingi unaofikia asilimia 63.

Kiwango hiki cha upungufu wa walimu ni kikubwa na hakikubaliki kwa nchi yetu ambayo ina vyuo vikuu na vya kati lukuki ambavyo vinatoa wahitimu wa mafunzo ya ualimu katika ngazi mbalimbali kila mwaka.

Taarifa hiyo inaonyesha kuwa Mkoa wa Mtwara, kwa mfano, kuna shule yenye wanafunzi 495, lakini ina mwalimu mmoja pekee.

Mwalimu mmoja kwa idadi hiyo ya wanafunzi ni kama vile shule haina kabisa mwalimu kwa kuwa inaweza kufungwa wakati wowote mwalimu akipata dharura itakayomfanya asiwepo kazini.

Hebu fikiria mwalimu huyo anafundishaje madarasa yote saba yenye watoto 495 tena ambao ni wa madarasa tofauti tofauti.

Taarifa hiyo pia inabainisha kuwa kuna shule za msingi 17 nchi nzima ambazo uwiano wa mwalimu na mwanafunzi unafikia mwalimu mmoja kwa wanafunzi zaidi ya 200.

Sambamba na taarifa hiyo, inaonyesha kuna shule 975 ambazo mwalimu mmoja anafundisha wanafunzi 100. Uwiano unaopendekezwa na mwongozo wa wizara ya sekta ya elimu ni mwalimu mmoja kwa wanafunzi 40 au 45.

Uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi 200 na kwingineko kwa wanafunzi 100 ni mkubwa mno. Uwiano huu haumwezeshi mwalimu kumfikia kila mwanafunzi kwa ukaribu ili kubaini matatizo yanayomkabili katika kujifunza. Mtoto huyu atarudi nyumbani akiwa mjinga kama alivyokuja.

Katika mazingira ya sasa ya kutoa elimu, nchi isitarajie kupata mafanikio makubwa kwani elimu yetu haitazamwi kwa jicho la nukuu ya Mandela ambapo pia anasisitiza, “hakuna nchi itakayopata maendeleo ya kweli kama watu wake hawajaelimika, kwani elimu ni sawa na hati ya kusafiri kwa ajili ya wakati ujao na kwamba kesho yetu inategemea mfumo bora wa elimu uliopo sasa.”

Lakini mimi ninasema tu kuwa upungufu wa walimu nchini ni kama wa kutengenezwa. Ninasema wa kutengenezwa kwa kuwa kuna idadi kubwa ya wahitimu wa kozi za ualimu katika ngazi mbalimbali wamejaa mitaani wanatafuta kazi wengine tangu mwaka 2015 lakini nafasi za ajira zinafunguliwa kwa kiwango kidogo.

Jeshi la wahitimu wa ualimu wasio na kazi, wangelikuwa ni bidhaa kama sukari, ningesema wafanyabiashara wameihodhi ili kutengeneza uhaba bandia kisha baadaye waje kuiuza kwa bei ya juu.

Inaendelea Uk. 33

# Upungufu wa walimu

Inatoka Uk. 32

Jeshi la wahitimu wa ualimu wasio na ajira ni kubwa. Miaka miwili au mitatu hivi iliyopita waliunda umoja ambao ulitikisa serikali hadi ikaomba kukutana na viongozi wao. Hata hivyo, baada ya uongozi kukutana na serikali pale Dodoma, umoja uko kimya kabisa. Umoja wa viongozi wa walimu wasio na ajira na serikali wanajua kilichojadiliwa.

Lengo la umoja wa walimu wasio na ajira uliundwa mahususi kupinga walichodai kuwapo kwa upendeleo mkubwa katika ajira za walimu na walitaka kuwepo uwazi.

Pamoja na kuwapo kikao cha umoja na serikali, bado tatizo la ajira kwa walimu tarajali lingalipo kwani wengi bado wako mitaani na vyeti vyao wakitafuta kazi.

Ninatamani vyuo vinavyotoa kozi ya ualimu vingesimamisha kudahili wanafunzi wa kozi hiyo angalau kwa miaka mitano ili kupunguza kukua kwa jeshi la walimu wasio na ajira nchini.

Kutokana na upungufu wa walimu, uwiano usiofaa kati ya mwalimu na wanafunzi hauna afya kabisa na kwamba unadumaza kiwango cha ubora wa elimu inayotolewa nchini hasa huko shule za msingi, ambako ndiko mwanafunzi anaanza kujengwa.

Kama mwanafunzi anajengwa kwa msingi usio imara, unadhani tunaweza kupata wasomi imara wa kuiendeleza nchi kweli?

Uwiano usiofaa kati ya mwalimu na wanafunzi umewakimbiza wazazi wenye uwezo kidogo kiuchumi na karibu viongozi wote wa umma kutoka ngazi zote kwa kuwapeleka watoto wao shule za msingi za binafsi ambazo angalau zinazingatia uwiano wa mwalimu na wanafunzi.

Tanzania inaweza kurekebisha hali hii kwa kuiga mfano wa Rwanda ambapo serikali hiyo imepiga marufuku viongozi wote wa umma kupeleka watoto wao kwenye shule za binafsi.

Kutokana na katazo hilo la Rwanda, serikali inaungalia mfumo wa elimu nchi humo kwa jicho la karibu, jambo ambalo limesaidia kuboresha mfumo wa elimu.

Hatua hiyo imeua shule nyingi za binafsi kwa kukosa wanafunzi na baadhi ya wamiliki wamekabidhi shule zao kwa serikali.

Ninasema tu, viongozi wetu haliwashughulishi sana suala la kuboresha elimu kwa kuwa walio wengi wakiwemo wabunge, mawaziri, madiwani na hata walimu wa shule za umma na wafanyakazi wa kawaida watoto wao wanasoma katika shule za binafsi ambazo zina walimu wa kutosha na wanazingatia uwiano wa mwalimu na wanafunzi.

Inashangaza zaidi kuona baadhi ya shule zetu kuna mrundikano mkubwa wanafunzi kwenye madarasa na kwingineko hata vitabu vya kiada ni taabu.

Tanzania haipaswi kuwa na upungufu wa walimu kwa kiwango kinachotajwa na taarifa ya Tamisemi.

Wahenga watakumbuka, katika kukabiliana na uhaba wa walimu miaka ya mwanzo wa uhuru, nchi iliomba msaada wa walimu kutoka India, Pakistan, Sweden, Marekani, Urusi, Uingereza na kwingineko ili kuziba pengo.


Wakati huo watoto wa viongozi wakuu walisoma shule hizi hizi za serikali ambazo sasa zimepewa jina baya la Saint Kayumba.

Serikali inashindwa nini wakati huu tukiwa na wahitimu lukuki ambao hawahitaji kulipiwa vibali vya ukaazi wala vya ajira.

Tatizo la walioko serikalini kwa mtazamo wangu unatokana na ukweli kuwa upungufu wa walimu haugusi elimu ya watoto wao.

Uwiano wa mwalimu na wanafunzi ulipo sasa, unafifisha ari ya mwalimu kufundisha na hivyo kushusha kiwango cha elimu nchini. Mara ngapi tunasikia kuna wafaulu wa darasa la saba kwenda sekondari wakiwa hawawezi hata kuandika majina yao kikamilifu.

Kama kuna mwalimu anayewajua wanafunzi wake kwa majina katika mazingira ya sasa ambapo darasa lina wanafunzi wanaofikia mia moja na hata zaidi, basi ni wale ambao huwa anawatuma mara kwa mara kwenda dukani na kwingineko.





Na Anti MSHAURI




# Fahamu misingi bora ya kuishi na jirani

NAKUSALIMU msomaji wangu wa safu ya uhusiano na karibu uweze kufahamu mambo mengi ya maisha.

Wiki hii nitakupa mbinu za kuishi kwa amani na jirani au mfanyakazi mwenzako.

Kuishi na jirani au mfanyakazi mwenzako kunahitaji hekima na uvumilivu kwa sababu nyinyi ni watu tofauti, lakini mnaishi au kufanya kazi pamoja kila siku.

Jambo la kwanza ni kuweka mipaka wazi tangu mwanzo. Mweleze mtu anavyopaswa kukutendea na wewe mwenyewe fanya hivyo.

Kwa mfano kwa jirani weka utaratibu wa saa za kelele na usafi, na kazini kila mtu ajue majukumu yake ili kuepuka mzigo kuangukia kwa mtu mmoja.

Pili, tumia mawasiliano ya moja kwa moja na ya heshima. Ukiona tatizo usinyamaze wala usiende kusengenya. Sema kwa upole na utulivu. Badala ya kulaumu sema unavyojisikia na unavyohitaji. Watu wengi huheshimu anayezungumza kwa ujasiri bila vurugu.

Tatu, jifunze kutoa na kupokea. Kuwa mtu wa kusaidia pale unapoweza lakini usiwe mzigo kwa wengine. Pia jifunze kupokea msaada ili mahusiano yasiwe ya upande mmoja.

Nne, epuka kabisa kusengenya na kuongea vibaya nyuma ya watu. Leo ukisema vibaya juu ya mwenzako, kesho watu hao watakusema wewe.

Kama mtu analeta habari za watu kuwa makini katika kutoa majibu na ikiwezekana usichangie mada maana ipo siku jambo hilo linaweza kukurudi.

Kubali tofauti. Ninyi hamuwezi kuwa sawa katika dini, tabia, kabila au mtindo wa kazi. Usijaribu kumfanya mtu awe kama wewe. Kumbuka kuwa amani inakuja unapojifunza kukaa na watu huku kila mmoja ana nafasi yake.

Lakini pia thamini na shukuru hasa kwa vitu vidogo unavyopewa. Neno asante, kutabasamu, au kuthamini msaada mdogo kunajenga daraja kubwa kati ya watu.

Watu wanakumbuka jinsi ulivyowafanya wajisikie zaidi ya maneno mengi.

Na mwisho, tambua wakati wa kujiondoa kwa heshima kwani sio kila mtu anastahili urafiki wa karibu.

Kama mtu ni mchonganishi, mvivu au hana heshima weka umbali wako. Kuwa mstaarabu lakini usijiuze ili kumpendeza kila mtu.

Lengo siyo kupendwa na kila mtu bali kuishi kwa amani, heshima na mipaka. Unapofanya hivyo nyumbani na kazini utapata utulivu na watu watakuheshimu.

***Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.***

# Lupita Nyong'o katika vazi la dhahabu



MWANAMITINDO na mwigizaji wa filamu kutoka nchini Kenya, Lupita Nyong'o, ameteka kapeti jekundu kwenye uzinduzi wa filamu ya "The Odyssey" jijini New York wiki iliyopita.

Lupita aliacha watu vinywa wazi kutokana na vazi lake lililosheheni dhahabu na vitu vya thamani ya juu sana.

Gauni hilo la kifahari la dhahabu ambalo halina kamba (strapless gold gown) kutoka kwa mbunifu Nicholas Oakwell Couture, limetengenezwa kwa urembo wa kina wa "lace" ya kishua.

Shingo yake ilipambwa kwa mkufu mzito wa lulu wa tabaka nyingi (layered pearl choker) wenye kito kikubwa cha dhahabu katikati ambayo imetengenezwa na mbunifu mashuhuri wa vito kutoka India, Sabyasachi. Muonekano huo wa Lupita umeratibiwa na kusimamiwa na stylist wake wa siku zote, Micaela Erlanger, huku yeye akimalizia kwa mtindo wa asili wa nywele zilizonyanyuliwa juu.

# Tumia karafuu kuondoa mikunjo

KARAFUU ina faida nyingi kwa afya na hata ngozi kwa kuwa ina utajiri mkubwa wa kuua sumu.

Pia huzuia mikunjo na kulinda afya ya viungo na ubongo dhidi ya magonjwa ya uzee.



**Matumizi;**

* Loweka karafuu nne hadi tano kwenye kikombe usiku kucha, halafu asubuhi uchuje na uweke kwenye chupa ya kunyunyizia, kisha nyunyizia kwenye uso au pakaa kwa kutumia pamba.

* Kunywa; Chemsha karafuu halafu unywe asubuhi kabla ya kula kitu chochote kwa sababu husaidia kusafisha mwili kutoka ndani.





# Lamata: Niliambiwa sitaweza kwa kuwa mwanamke

**Na Mwandishi WETU**

MUONGOZAJI wa tamthilia nchini, Lamata Leah, amefunguka sababu ya kuwaunga mkono na kuwapa nafasi wanawake wengi katika sekta ya filamu.

Lamata amesema wakati anaanza safari hiyo ya kuongoza tamthilia, alikatishwa tamaa mara nyingi huku akiambiwa hataweza kwa sababu ni mwanamke.

Pamoja na kukatishwa tamaa, msanii huyo leo amegeuza maumivu hayo kuwa nguvu ya kuwainua wanawake wengine.

"Hata wanaume ninawasaidia lakini asilimia 70 ya ninaowasaidia ni wanawake. Hii inatokana na safari yangu katika tasnia kwani wakati naanza nilikatishwa sana tamaa lakini nilipambana hadi nikafika hapa. Hivyo ninajisikia fahari zaidi ninapomwinua mwanamke,"amesema Lamata.

Kwa sasa, Lamata ni miongoni mwa waongozaji wa tamthilia wanaoheshimika zaidi nchini, akithibitisha kuwa uwezo hauna jinsia, bali unahitaji nafasi na uthubutu.

# Marioo, Paula wamefunga ndoa?

**Na Mwandishi WETU**

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Marioo amezua gumzo mtandaoni baada ya kuposti picha kwenye ukurasa wake wa Instagram ikimuonyesha katika mazingira yanayoashiria tukio la ndoa.

Huku akiambatanisha picha, Marioo aliandika ujumbe mfupi: "Alhamdulillah… Jumaa Kareem," huku Paula, ambaye ni mama wa mtoto wake, akitoa maoni kwenye post hiyo kwa kuandika, "Mashallah mume wangu."

Chapisho hilo limezua hisia na maswali kutoka kwa mashabiki kuhusu uwezekano wa wawili hao kuingia kwenye ndoa rasmi, ingawa hadi sasa hakuna taarifa rasmi iliyotolewa na Marioo au Paula kuthibitisha suala hilo.




Bati/ Mtu, Mtu Bati
HATUCHOKI!
Changia kupitia
NMB A/C NO 31910046325
ELCT KARAGWE IRON SHEET PROJECT
CRDB A/C NO 0150764151900
UWAKILI PROJECT ELCT KAD
Mawasiliano:
0754 742 423
Askofu Benson K Bagonza



# Usajili haujapoa Simba, Yanga



*Kelvin Nashon*

**Na Mwandishi WETU**

VIKUMBO vya dirisha la usajili la msimu wa 2026/27 vimeanza rasmi sasa huku timu kubwa zikitambiana ubora wa kupata maingizo mapya ya wachezaji.

Vilabu viwili vikubwa vya Tanzania; Simba na Yanga, kama kawaida usajili wao umekuwa mjadala mkubwa mitaani, redioni, na mitandaoni.

Wababe wa Msimbazi, Simba wameanza mapema. Uongozi umeweka wazi kwamba lengo lao kubwa msimu huu ni kutawala ndani ya nchi na kwenda mbali katika mashindano ya CAF.

Msisitizo mkubwa umekuwa katika kuleta wachezaji wenye uzoefu wa kimataifa, hasa katika maeneo ya ulinzi, kiungo na ushambuliaji.

Kocha Mkuu wa Simba, Steve Barker amesema; “Tunataka kikosi chenye ushindani. Siyo tu kushinda ligi, bali kupambana hadi hatua za nusu fainali Afrika.”

Jana Simba walimtambulisha kiungo mkabaji, Kelvin Nashon ambaye amejiunga na Wekundu hao akitokea Pamba Jiji ya Mwanza kwa kandarasi ya miaka miwili.

Mchezaji huyo anakuwa wa kwanza kutambulishwa katika dirisha hili na Mnyama Simba, huku tetesi zikisema kuna uwezakano wa kudondoka kwa mshambuliaji wa zamani wa Mamelodi ya Afrika Kusini, Peter Shalulile na winga kutoka nchi hiyo, Keletso Makgalwa ambaye anakipiga Klabu ya Sekhukhune United kwa mkataba wa miaka miwili.

Kwa Upande wao, mabingwa wa kihistoria - mara tano mfulululizo, Yanga nao hawapoi, hawaboi wameshusha mashine mpya kinda kutoka Fountain Gate, Juma Abushiri maarufu ‘Chuga Boy’ ambaye amejiunga na mabingwa hao kwa kandarasi ya miaka mitatu.

Pia, zipo tetesi kwamba timu hiyo kutoka Jangwani, Dar es Salaam huenda ikamtambulisha muda wowote, kiungo mshambuliaji wake wa zamani, Stephane Azizi Ki.

Timu ya Azam nayo haipo kinyonge kwani wamemtambulisha mshambuliaji Kipre Jr pamoja na beki wa kati, Henri Stanic kutoka Stellenbosch ya Afrika Kusini.

Ikumbukwe Azam wameshika nafasi ya tatu msimu uliopita na wamepania kufanya mapinduzi msimu unaokuja katika ligi na michuano ya kimataifa.

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS' ASSOCIATION